# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Septemba 8, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581793

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Ng'arisha uso kwa 'Make Up'

UKURASA 14

UKURASA WA 3

**Ziara** Makalla ilivyoibua utitiri wa kero Arusha



UKURASA WA 3

**Serikali** yaanika mikakati katika kukabili uhaba fedha za kigeni



UKURASA WA 5

**Majaliwa** ataja mageuzi huduma za afya watoto wachanga

## Mongella ataja manufaa misaada, mikopo toka nje

UK. 5

RIPOTI MAALUM

# Uporaji wa simu, mikoba kwa bodaboda watisha

• **Waliopigwa** wasimulia madhila, polisi yatajwa, TCRA yatoa neno... *Uk. 4*

## YALIYOMO

UKURASA 8

### SERIKALI YAWATOA HOFU WALIOANDIKISHWA 2015

SERIKALI imewatoa hofu wananchi walioandikishwa kupiga kura mwaka 2015 na mwaka 2019/20 kuwa kadi zao ni halali na zitatumika katika Uchaguzi Mkuu, 2025. Imesema uboreshaji wa Daftari la Kudumu la...

## Masauni atetea uamuzi wa kufukuzwa 'Kiboko ya Wachawi'

UKURASA 2



Dk. Bakari Jabir

## Polisi yaanza uchunguzi wa kutekwa kigogo CHADEMA

UK. 2

MICHEZO **GAMONDI AIWEKA CBE KIGANJANI MWAKE** UK.24

MAONI, UK.6

# Waziri Masauni atetea uamuzi kumfukuza 'Kiboko ya Wachawi'

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema kitendo chake cha kumfukuza Kiongozi na Mchungaji wa Kanisa la Christian Life maarufu kama Kiboko ya Wachawi, Dominique Dibwe, kilikuwa sahihi kwa sababu mhusika amedhihirisha utapeli kupitia video mbalimbali zilizoko mtandaoni.

Katika mitandao ya kijamii kumesambaa video fupi za mchungaji huyo ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zenye maudhui ya kejeli akionekana akihesabu fedha, huku akisema bado anakumbuka Sh. 500,000 alizokuwa akiwatoza waumini wake ili kuwaombea.

Julai 25, mwaka huu, serikali kupitia Msajili wa Jumuiya za Kiraia, Emmanuel Kihampa, ilimwandikia barua mchungaji huyo kumtaka kufunga shughuli na huduma alizokuwa akiziendesha huko Buza, Temeke mkoani Dar es Salaam, agizo ambalo lilitekelezwa.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, aliyasema hayo jana wakati akifunga makambi yaliyoandaliwa na Kanisa la Waadventista Wasabato Maranatha katika Mtaa wa Majani ya Chai, Arumeru, mkoani Arusha kwamba walimwondoa mchungaji huyo kutokana na kukiuka sheria ya usajili.

"Nimeshuhudia huko alikokwenda amekuwa akisambaza klipu za video kuthibitisha kwamba aliyokuwa akifanya ni kinyume kabisa na mafundisho ya kitabu cha dini.

"Ikiwamo suala la kutapeli watu, kuwatoza fedha nje ya utaratibu, kuwaaminisha watu kwamba miujiza inaweza kuwafanya wawe matajiri au wapate ufumbuzi wa matatizo yao, mambo ambayo ni kinyume na mafundisho ya dini zetu" alisema.

Masauni alipongeza Kanisa la Waadventista Wasabato kwamba wao si sehemu ya wanaohubiri mambo kama hayo.

Aliwapongeza kwa kusimamia misingi sahihi ya vitabu vya dini na kutoa wito kwa watu walioingia katika shughuli za kidini, kufuata misingi ya kisheria inayolenga kuhakikisha inafuata mafundisho sahihi ya vitabu vya dini.

"Uhuru wa kuabudu kwa mujibu wa katiba upo, lakini hautakiwi kuvuka mipaka na kuvunja sheria za nchi si kwa wageni hata wenyeji. "Ziko sheria lazima zifuatwe zimetungwa kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa taifa hili," alisema.

**MAUAJI NA UTEKAJI**

Pia alisema suala la maadili kwa vijana ni muhimu, akibainisha katika kipindi cha mwezi Agosti hadi sasa, wameshuhudia ongezeko la matukio mabaya yanayohusu mauaji ya kikatili yanayohusishwa na masuala mbalimbali, ikiwamo imani za kishirikina.

"Tumesikia mauaji yaliyochanganyika na uhalifu mwingine ukiwamo ubakaji, uuaji wa kutumia silaha za jadi na upoteaji. Imechukua kazi kubwa sana vyombo vyetu vya usalama kufanya udhibiti wa jambo hilo, yote yanachangiwa na mmomonyoko wa maadili.

"Hakuna hata mtu mmoja ambaye ana hofu ya Mungu ambaye atafanya kitendo chochote kiovu kinacholenga kuleta athari au madhara kwa watu wengine. Dini zote zinakataza," alisema.

Hivi karibuni, Jeshi la Polisi lilitangaza kuwashikilia watu kadhaa akiwamo mganga wa kienyeji huku miili 10 ikibainika baadhi kuzikwa kwa mfumo wa kukaa wakiwamo watoto wa watuhumiwa, baada ya watu hao kuripotiwa kupotea na wengine kutekwa.



Msukuma toroli akiwa amepakia bidhaa zake akitafuta wateja katika mji wa Kondoa hivi karibuni. PICHA: JUMANNE JUMA

# Polisi yaanza uchunguzi wa kutekwa kigogo CHADEMA

**Na Halfan Chusi**

JESHI la Polisi nchini limesema limeanza uchunguzi dhidi ya tukio la Mjumbe wa Sekretarieti ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ally Kibao, anayedaiwa kutekwa wakati akisafiri kwa basi la Tashrif.

Jana, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alitoa madai hayo mbele ya vyombo vya habari, huku Msemaji wa Jeshi la Polisi, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), David Misime, akieleza kuanza kwa uchunguzi huo.

Katika taarifa yake, Misime alisema kuna taarifa zimesambaa katika mitandao ya kijamii zikieleza kuwa juzi jioni maeneo ya Tegeta, Dar es Salaam, Kibao akiwa safarini na basi la Tashrif, alishushwa na kuchukuliwa na watu wasiojulikana majina yao.

"Leo (jana) tumesikia taarifa kuhusiana na tukio hilo kupitia vyombo vya habari iliyotolewa na Mnyika. Jeshi la Polisi lingependa kutoa taarifa kuwa lilipokea taarifa hiyo na kuanza uchunguzi wa kubaini kilichotokea, chanzo chake na watu waliohusika ni akina nani," alisema Misime katika taarifa hiyo.

Awali, akizungumzia tukio hilo, Mnyika alilitaka jeshi hilo kueleza aliko Kibao.

Mnyika alisema alipokea taarifa za tukio hilo juzi saa 12 jioni za madai ya kutekwa kwa Kibao katika eneo la Kibo Complex Tegeta, alipokuwa akisafiri kuelekea Tanga anakoishi.

"Akiwa amepanda basi la Tashrif lenye namba za usajili T 343 EES, lilipofika maeneo hayo likazuiwa na magari mawili nyeupe aina ya Toyota Landcruiser na gari dogo lingine yakiwa hayana nembo yoyote.

"Wakashuka watu kutoka humo wakiwa na silaha moja kati yao akaenda katika kioo cha mbele kwa dereva, wawili wakaingia ndani, wengine wakabaki nje walikwenda moja kwa moja katika siti yake wakamchukua kwa nguvu.

"Wakati wanashuka akaongezeka mwingine mmoja aliyekuwa ndani ya gari whilo akaungana na wenziwe na kwa taarifa nilizonazo wakati wanamshusha walimpiga," alidai Mnyika.

Katibu Mkuu huyo alisema mpaka sasa hawajui mwenzao yuko wapi na ana hali gani.

"Tumetuma mawakili wa chama Kituo Kikuu cha Polisi ili tujue yuko wapi, lakini mpaka sasa hatujapata taarifa yoyote ya wapi yupo. Nitoe wito kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi aeleze iwapo alitekwa, sababu za kumteka, yuko wapi na ana hali gani," alisema.

Mnyika alisema msimamo wa chama kutokana na uzito wa kushamiri kwa vitendo hivyo mathalani uchaguzi unapokaribia, wameanza maandalizi ya kikao cha chama ili kutafakari hali ya usalama nchini na kufanya uamuzi wa pamoja na kisha wataeleza hatua watakazochukua.

# WMA, TAKUKURU zatekeleza maagizo

**Na Veronica Simba,**
DODOMA

Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Dodoma imetoa elimu ya vipimo kwa watumishi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuzitaka mamlaka na taasisi za umma kupanga na kutekeleza kwa pamoja majukumu mbalimbali ya serikali.

Akifungua semina hiyo ya siku moja iliyofanyika juzi mjini hapa, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Kaspar Mmuya, alipongeza ushirikiano wa taasisi hizo mbili unaolenga kutekeleza maelekezo ya Rais ya kuwahudumia wananchi ipasavyo.

"Nimefurahishwa na ushirikiano wa taasisi hizi mbili wenye lengo la kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhusu dhana ya kufikiri kwa pamoja na kutenda kwa pamoja kama serikali," alisema.

Mmuya aliwataka washiriki kutumia semina hiyo kupambanua endapo kuna upungufu wowote katika Sheria ya Vipimo inayosimamiwa na WMA na kutafuta suluhisho la pamoja ili kuboresha utekelezaji.

Pia aliitaka WMA kuendelea kutoa elimu ya vipimo kwa wafanyabiashara na watumiaji wa bidhaa ili pande zote mbili zipate kilicho stahiki. Pia aliongeza kwamba katika utoaji elimu, wakulima waeleweshwe kuachana na utamaduni wa kutumia madalali bali wauze mazao yao katika maghala.

"Rais ametoa maelekezo kwamba mazao yauzwe kwenye maghala na huko kwenye maghala kuwe na mizani ambayo imekaguliwa na kuhakikiwa na Wakala wa Vipimo ili kumlinda mlaji na mfanyabiashara," alisema.

Mmuya alitoa wito kwa wafanyabiashara, walaji wa bidhaa na huduma mbalimbali kuzingatia matumizi ya vipimo sahihi na kuwakumbusha kwamba sheria ya vipimo imewapa WMA mamlaka ya kutoza faini kwa yeyote atakayekiuka mwongozo wa sheria hiyo.

Pia alizitaka WMA na TAKUKURU kuwa mfano kwa sheria wanazozisimamia na kuchukuliana hatua baina yao endapo kutabainika ukiukwaji wa sheria.

"TAKUKURU, mtumishi yeyote wa WMA akitenda ndivyo sivyo kwa kujihusisha na rushwa basi achukuliwe hatua. Vivyo hivyo kwa WMA, mkibaini mtumishi wa TAKUKURU anajihusisha na uvunjifu wa sheria ya vipimo katika shughuli zake kama Mtanzania wa kawaida ikiwamo kilimo, biashara na nyinginezo, msisite kumchukulia hatua," alisisitiza.

Meneja wa WMA Mkoa wa Dodoma, Karim Zuberi, alisema lengo la kutoa semina hiyo kwa watumishi wa TAKUKURU ambao ni watumiaji wa vipimo, ni kuwapatia uelewa ili wajue haki zao wanaponunua bidhaa au kupata huduma mbalimbali.

"Kupitia semina hii watapata uelewa ni kwa namna gani kipimo kinatakiwa kuwa kabla, wakati na baada ya kununua bidhaa au kupata huduma," alisema Zuberi.

HABARI KITAIFA

# Serikali yaanika mikakati katika kukabili uhaba wa fedha za kigeni

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema inaendelea kuweka mikakati na mbinu mbalimbali katika kushughulikia uhaba wa fedha za kigeni (Forex).

Mikakati hiyo ambayo inalenga muda mfupi, wa kati na mrefu, ni pamoja na kuainisha baadhi ya sekta ambazo zinaweza kuleta mapato zaidi ambayo yatatoa suluhisho la kudumu la uhaba wa fedha za kigeni.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, aliyasema hayo jana alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi mpya wa Uingereza nchini, Marrianne Young, aliyefika ofisini kwake, Dodoma kwa ajili ya kujitambulisha.

Dk. Nchemba alisema kuwa katika bajeti inayoendelea, serikali imeweka vipaumbele kwa baadhi ya sekta ambazo ni za kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

"Japokuwa kama nchi kuna hali tofauti na baadhi ya nchi nyingine zinazoizunguka Tanzania kwa kuwa inatekeleza miradi mikubwa ya kimkakati," alisema.

Alisema hali hiyo imesababishwa na kutokuwa na uwiano katika uingizaji wa bidhaa nchini na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi, lakini pia imetokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati kama mradi wa kuzalisha umeme wa Bwawa la Nyerere, mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) na Daraja la Busisi.

"Ni wazi kwamba kila unapokuwa na tofauti yoyote kati ya kile unachouza nje na kile unachoagiza kutoka nje, kutakuwa na shinikizo katika fedha za kigeni na hicho ndicho kinachotokea. Pia mikakati na hatua zinazochukuliwa zitasaidia kupata suluhisho la kudumu siku za karibuni," alisema.

Waziri huyo wa fedha alitumia fursa hiyo kumpongeza Young, kwa kuteuliwa kuwa Balozi wa Uingereza nchini na kuahidi kuendelea kufanya kazi pamoja ili kuendeleza ushirikiano kati ya nchi hizo katika kuhakikisha maendeleo endelevu ya kiuchumi. "Dhamira ya serikali ni kuendelea kushirikiana na Serikali ya Uingereza ili kuimarisha ushirikiano muhimu wa maendeleo," alisema.

Dk. Nchemba alisema Uingereza ni mdau muhimu wa maendeleo kwa kuendelea kutekeleza ajenda ya Maendeleo ya Kitaifa kama ilivyoainishwa chini ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 (FYDP III).

"Tunashukuru sana kwa msaada thabiti ambao Serikali ya Uingereza imekuwa ikitoa kwa Tanzania, hususan katika maeneo ya ulinzi wa kijamii kupitia Mpango wa TASAF awamu ya II, Sekta ya Elimu, Afya kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya na Msaada wa Mpango wa Kupambana na Rushwa ambao umechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo endelevu ya kiuchumi nchini Tanzania" alisema.

Balozi Young, alimshukuru Waziri wa Fedha, kwa kumkaribisha na kuahidi kuendeleza ushirikiano kati yao katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya kiuchumi kwa Tanzania.

"Ningependa kuwapongeza kwa sera imara za uchumi wa jumla na maendeleo. Ninaelewa kwamba tumekuwa na msaada wa muda mrefu kutoka Mamlaka ya Mapato na Forodha ya Uingereza (HMRC) katika eneo hili na tunafanya kazi zaidi ili kusaidia juhudi za Serikali ya Tanzania za kuongeza wigo wa mapato" alisema.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Madeni Wizara ya Fedha, Japhet Justine, viongozi waandamizi wa Wizara ya Fedha na maofisa kutoka Ubalozi wa Uingereza.



Wanafunzi wa kike katika Shule ya Msingi Iboni, iliyopo Wilayani Kondoa Mkoani Dodoma, wakining'inia kwenye tawi la mti uliopo shuleni hapo jambo ambalo ni hatari kwa usalama wao hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ziara ya Makalla ilivyoibua utitiri wa kero

**Na Salome Kitomari,** KARATU

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, ametatua kero 60 za wananchi wa Longido na Karatu na kuunda kamati kila wilaya ya ufuatiliaji ili kila mwananchi aliyewasilisha jambo lake lipatiwe ufumbuzi wa kudumu.

Usikilizaji na utatuzi wa kero za wananchi unaofanywa na kiongozi huyo kila anapokwenda, hutanguliza maofisa wa chama kusikiliza wananchi na kurekodi kero zao ambazo kupitia mkutano wake wa hadhara kila jioni husomwa na mtaalam hueleza hatua zilizochukuliwa.

Miongoni mwa kero ambazo zimejirudia katika mikutano yake ni zinazohusu ukosefu wa maji na kukatikatika kwa umeme, hali inayowafanya wananchi kushindwa kufanya shughuli za uzalishaji.

Akiwa Longido wanachama wa CCM, walisema kuna mradi wa maji wa muda mrefu wa kutoa maji Mto Simba ambao bado haujakamilika, huku Mji wa Longido ukiwa na shida kubwa ya huduma hiyo muhimu.

Suala hilo lilijitokeza pia, Kilimahewa Kata ya Mundarara, kwenye mkutano wa hadhara ambapo kila kiongozi wa chama na mbunge walivyopanda jukwaani, walieleza kero kubwa ni ukosefu wa maji na kumwomba kuitatua.

Kwenye mkutano wa hadhara Karatu mjini, kila aliyepanda jukwaani, alitaja kero hiyo kuwa imetokana na mafuriko yaliyoharibu miundombinu.

"Katika mji wetu wa Karatu kuna tatizo kubwa la maji baada ya miundombinu kuharibiwa na mafuriko. Wananchi unaowaona hapa shida yao kubwa ni maji," alisema Mbunge wa Karatu, Daniel Awack, huku akishangiliwa na wananchi.

Kutokana na kilio hicho, Makalla alimpigia simu mara tatu Waziri wa Maji, Juma Aweso, akiwa kwenye kikao na viongozi wa chama, Mundarara na Karatu ambaye pamoja na kuahidi kushughulikia, alisema atafanya ziara maeneo hayo.

"Komredi Makalla maelekezo yako ni amri kwangu. Nitakwenda Longido na Karatu. Tunashughulikia kero ya maji, tulifanya tathmini ya awali katika mji wa Karatu na kubaini kuna visima vilipata hitilafu. Ninamwelekeza Katibu Mkuu ndani ya wiki moja, tutaleta Sh. milioni 100 kurekebisha ili huduma irejee," aliahidi.

Aweso alisema kuna mradi mkubwa wa zaidi ya Sh. bilioni nne unatekelezwa wilayani humo na kuwataka viongozi kusimamia vyem, ili kila shilingi iingie katika kutekeleza mradi huo na kuondoa tatizo la maji.

Alisema katika eneo la Longido, tayari mradi wa kutoa maji Mto Simba umeshakamilika na hatua inayofuata ni kuyasambaza katika Mji wa Longido. Aweso aliwataka wananchi hao kuendelea kuiamini CCM kwa kuwa kwenye Ilani yake kuna utatuzi wa kero za wananchi.

Kero nyingine iliyoibuka ni kukatikatika kwa umeme ambayo Makalla alipotembelea Shule ya Sekondari ya Wasichana Longido Samia, aliona taa za sola ni nyinyi na alipouliza aliambiwa kuna tatizo la umeme.

"Wakati ninatembelea majengo ya shule hii, nimeona taa za sola nyingi, nimeelezwa kuna tatizo la umeme. Tunawaagiza TANESCO walishighulikie," alisema Makalla.

Akiwa Longido Mundarara, alielezwa tena tatizo hilo ambako kote alimwita Kaimu Meneja wa TANESCO Mkoa wa Arusha, Adelhem Mkulu, ambaye alisema njia ya umeme imelemewa kwa kuwa inahudumia umbali wa kilomita 1,000, hivyo kujengwa kituo cha kupooza umeme eneo la Karatu ili kuwezesha umeme kuwafikia bila tatizo.

Kero nyingine ni wananchi waliopisha upanuzi wa uwanja wa ndege Manyara unaotarajiwa kuanza Septemba, mwaka huu, kutolipwa mapunjo ya fidia iliyochelewa.

Mwakilishi wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Arusha, alisema tayari wameshaandikia na mchakato unaendelea Wizara ya Fedha. Alisema fedha zilizolipwa ndio stahiki ya wananchi na hakuna aliyepunjwa kutokana na mtathmini wa serikali kupitisha na kuridhia.

Alisema kwa yeyote ambaye hakuridhika basi anapaswa kumwona Mkuu wa Wilaya ambaye ndiye mwenyekiti wa kamati ya tathmini.

Kero nyingine ni barabara kati ya Longido na Mundarara, Kigongo hadi Sale inayokwenda wilaya ya Ngorongoro, ambayo imeharibika na kuwafanya wananchi washindwe kusafiri kuzifikia huduma muhimu.

Pia wilayani Karatu nako walieleza kuwa kero kubwa ni barabara nyingi kuharibika na kuomba kujengwa za kiwango cha lami, ambapo Mwakilishi wa TANROADS alisema kuwa serikali imetenga fedha za ukarabati na ujenzi wa barabara kuhakikisha zinapitika ikiwamo kujenga madaraja.

Kuhusu kero iliyoibuliwa kuwa wazee kutozwa fedha wanapokwenda kupata matibabu licha ya Sera ya serikali kuelekeza kundi hilo matibabu ni bure.

Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, alithibitisha kwamba walipokea malalamiko ya wazee hao na kwamba wengi huhitaji huduma za kibingwa ambazo hazipo katika ngazi ya wilaya, jambo ambalo linakuwa ni changamoto kuwahudumia.

Kero nyingine zilizoibuliwa zinahusu migogoro ya ardhi, ukosefu wa ajira, ndoa za ututoni ,kuziba kwa mifereji ya maji, mume kutelekeza familia baada ya kuuza mali, aliyenunua kiwanja kunyimwa njia na aliyemuuzia, wastaafu kupunjwa fedha zao, kutolipwa mishahara ya miezi mitatu na mwajiri.

Katika wilaya zote alizopita, Makalla aliwaelekeza wakuu wa wilaya husika kuandika mukhtasari wa kero zote na majibu yaliyotolewa, yakiwa nan amba za simu za walalamikaji kisha zifikishwe kwake kwa ajili ya ufuatiliaji.

RIPOTI MAALUM

# Uporaji simu, mikoba kwa bodaboda watisha



Na Waandishi Wetu

HALI inatisha. Ndiyo hali halisi kutokana na wimbi la uporaji wa mikoba, simu na vitu vingine vya thamani unaofanywa na baadhi ya waendesha bodaboda kurejea kwa kasi katika miji mbalimbali, hivyo kuzua taharuki kwa wananchi.

Kwa wanaopora simu, wamekuwa wakituma ujumbe mfupi wa kuomba fedha za dharura kwa kutumia namba zilizoko katika siku iliyoibwa na baadhi bila kujua hulizwa.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe hivi karibuni katika maeneo mbalimbali nchini, umebaini matukio hayo hufanyika bila kujali ni mchana au usiku. Wengi wanaoibiwa ni wale wanaotembea kwa miguu au wanaokuwa kwenye bodaboda au bajaji.

Wahalifu hao wamekuwa wakipakizana wawili katika bodaboda na abiria wake ndiye hutekeleza uporaji huo, huku baadhi ya wanaoibiwa wakiachwa na majeraha kutokana na kuvutwa kwa nguvu na ghafla.

**WALIVYOLIZWA**

Renatus Mahima, mkazi wa Kimara, Ubungo mkoani Dar es Salaam, anayefanya kazi kwenye kiwanda kimojawapo Mikocheni, anasilimulia kilichomsibu Agosti 24, mwaka huu.

"Nilitoka ofisini majira ya saa 1:00 usiku nikatembea mpaka Mwenge Mpakani, kiliko kituo cha daladala na bajaji, nilipofika pale nikachukua bajaji za kwenda Mbezi. Ndani ya bajaji tulikuwa abiria wanne, nilikuwa nimekaa siti ya nyuma na wanawake wawili, mimi nikiwa mlangoni na mbele alikuwako abiria mwingine mtu wa makamo.

"Nilitoa simu mfukoni ili kusoma ujumbe niliotumiwa kwenye simu. Tulipokaribia kituo cha Mlimani City ghafla ikatokea bodaboda nyuma ikiwa katika mwendokasi. Walikuwa wamepakizana wawili, yule wa nyuma akavuta simu, wakanivuta na mimi nikaanguka kutoka katika bajaji," anasimulia.

Mahima anasema bahati nzuri baada ya kudondoka nyuma hakukuwa na gari lakini aliumia kwa kuchubuka mkono wa kulia na magoti yote.

"Dereva wa bajaji alinisubiri na ndiye aliyenisaidia simu yake nikapiga simu kampuni husika wakazima laini. Laini ya mtandao wa simu nyingine sikuizima kwa wakati ule mpaka nilipofika nyumbani kwa sababu sikupata mtu mwenye namba ya kampuni hiyo," anasema.

Anasema saa moja na nusu baadaye alipotumia kompyuta mpakato kufuatilia simu yake, alibaini tayari iko maeneo ya Chamazi, Temeke mkoani Dar es Salaam.

Hata hivyo, anasema hakutoa taarifa polisi wala Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), zaidi ya kufuta taarifa zake zote katika simu kwa kutumia kompyuta yake.

"Kuna namna ya kufuta taarifa zako kwenye simu kwa kutumia IMEI (International Mobile Equipment Identity) ya simu au gmail uliyokuwa unatumia kufungua mafaili kwenye simu," anasema.

IMEI ni namba ambazo zinakuwa kama utambulisho wa kifaa na katika simu, mara nyingi zinakuwa na tarakimu 15 na huwa hazifanani zinakuwa katika kifaa kimoja tu. Pindi mtu akiibiwa kifaa au simu huwezesha kufuatilia nyendo za simu hiyo kama ikiwa imeunganishwa na intaneti na kuweza kufuta kila kitu na kuifunga kabisa simu hiyo kutumika tena kupitia IMEI ya simu hiyo.

Mkazi wa Mwenge, Dar es Salaam, ambaye hakutaka majina yake kuandikwa gazetini, anasimulia kuwa mwaka jana, aliibiwa simu yake majira ya asubuhi eneo la Sinza Mapambano, wakati akizungumza na mwendesha bodaboda wapi ampeleke.

"Wakati ninajiandaa kupanda huyo mtu wa bodaboda aliondoa ghafla bodaboda yake akiwa ameiba simu yangu na kuniacha. Muda mfupi mbele watu wangu wa karibu wakaanza kutuma ujumbe wa kuombwa fedha kuanzia Sh. 200,000 hadi Sh. milioni moja na wapo waliotuma.

"Kama hiyo haitoshi walichukua fedha kwenye akaunti Sh. milioni sita. Nilitoa taarifa polisi na kila nilipofuatilia nilikuwa ninaambiwa subiri mpaka nikaamua kuacha ," anasema.

Akitaja namba walizotumia kuhamishia fedha hizo baada ya kufanya wizi kwenye akaunti yake alisema ni 0769860535, 0716986400 na 0699147562.

Mkazi wa Makumbusho, Dar es Salaam, Remi Kibago, anasema hivi karibuni ameshuhudia maeneo ya Mikocheni B, bodaboda wakikwapua pochi ya mwanamama aliyekuwa amesimama pembezoni ya barabara kisha kuondoka nayo.

"Asilimia kubwa wenye tabia kama hizo hata mtaani wanajulikana. Kikubwa Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na raia wema wafanye msako wa kuwatafuta vijana wote wanaojihusisha na vitendo hivyo," anasema.

Mariam Salehe, anasema mbinu ambazo wahalifu hao hutumia ni kuangalia eneo lenye upenyo mkubwa ili wasikamatwe.

"Baadhi wanatembea na panga wakiona hakuna watu wengi, dereva anasimama alafu abiria wake ambaye ni mhalifu mwenzake anashuka na kutumia panga kutishia ili utoe simu, fedha au chochote cha thamani kisha wanaondoka," anasema.

Mkazi wa Mtaa wa Bukoba, Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera, Hellen Joackim, anasema wizi unaohusisha waendesha bodaboda umekua kwa kasi hivi sasa.

"Wizi huu unafanyika kwa njia tofauti, kwa kumkwapua mwenda kwa miguu alichonacho au wanapopakia abiria kukusafirisha sehemu moja kwenda nyingine njiani anaibiwa kila alichonacho kisha anatelekezwa," anasema.

Mkazi wa Kata ya Miembeni, Aidan Heleman anasema: "Mei, mwaka huu, majira ya saa 5:00 usiku nilichukua bodaboda anipeleke nyumbani, ile tumefika nilipompa Sh. 5,000 ili akate Sh. 2,000 yake akatokomea na fedha yote."

Mwendesha bodaboda wa mjini Bukoba, Josephat Katwale, anasema matukio hayo yako kwa vijana ambao sio waaminifu na hasa hutokea nyakati za usiku.

Jijini Arusha, baadhi ya wananchi akiwamo Andrew Daniel, wamesema matukio hayo yalipungua baada ya waliokuwa wakikamatwa kuchomwa moto, lakini hivi sasa yamerejea kutokana na wananchi kuacha kuchukua hatua mkononi.

Hamis Ramadhani, mwendesha bodaboda jijini humo, anasema, "Wizi unaofanywa na baadhi ya wanaotumia bodaboda, lawama hurudi kwetu wakati wengine hatuhusiki."

Katibu wa Chama cha Waendesha Bodaboda mkoani Manyara, Athuman Shaban, anasema matukio ya wizi yalikuwapo kipindi cha nyuma ila kwa sasa yamedhibitiwa mkoani humo.

Mkoani Kilimanjaro, wizi wa kutumia bodaboda unalalamikiwa zaidi kutikisa katika Manispaa ya Moshi na Wilaya ya Hai, ambapo mfanyabiashara Baraka Hussein, anasema huhusisha zaidi wizi wa simu, pochi na vitu vingine vya thamani kama cheni za dhahabu na za fedha.

Katika Mji wa Hai, Onesmo Kimaro, anasema upande wao baadhi ya bodaboda hutumika kubeba mifugo ya wizi kama nguruwe na mbuzi hasa nyakati za usiku.

**WAJITETEA**

Dereva bodaboda wa eneo la Makumbusho, Rasul Musa, anasema wanaofanya matukio hayo si bodaboda waliosajiliwa bali ni wezi wanaotumia vyombo hivyo kuchafua tasnia hiyo.

"Haiwezekani kama kwa siku mtu unapata mpaka Sh. 30,000 kwa kubeba abiria halafu tena ushawishike kwenda kuiba kitu cha mtu. Haiingii akilini kabisa hao wanaofanya hivyo ni wezi," alisema.

**WATOA USHAURI**

Jabiri Mtumba, ameishauri serikali kuharakisha mpango wake wa ufungaji kamera za CCTV katika Barabara, ili iwe rahisi kubaini matukio ya uhalifu yanapotokea na wahusika kukamatwa.

Pia anasema kamera hizo zikiwamo maeneo mengine ya mtaani katika makazi ya watu zitasaidia kupunguza matukio hayo kwa sababu wataogopa kujulikana.

Gift Mtyauli, aliishauri serikali kuwasajili bodaboda kwa namba ili iwe rahisi kutambuliwa iwapo atafanya uhalifu.

Baadhi ya wakazi mkoani Kagera na Mwanza wameiomba serikali kuweka utaratibu maalum wa kuwatambua bodaboda wote nchini ili kudhibiti matukio hayo na mengine.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi hao akiwamo Vanessa Michael, mkazi wa Mwanza, anasema hatua hiyo ndio mwarobaini wa vitendo hivyo vinavyoendelea katika baadhi ya maeneo.

Akizungumza kwa niaba ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Ofisa Mnadhimu Kamishna Msaidizi (ACP) Yussuf Daniel, alikiri kupokea kesi za namna hiyo na wanaendelea na utaratibu kuona njia sahihi ya kuzikomesha.

Daniel aliwataka wananchi kutoa taarifa za wote ambao wanawatilia mashaka na kuwa na ushahidi wa kuhusika na matukio hayo ili waweze kuyakomesha.

Alipotafutwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Rolf Kibaja, alisema anafahamu kuwapo kwa matukio hayo lakini vitendo hivyo hushughulikiwa na Jeshi la Polisi.

"Huwa tunapokea malalamiko kwa watu mbalimbali kuhusu kuibiwa simu, lakini sehemu sahihi kwa malalamiko yao ni polisi kwa sababu wao ndio wanahusika na wizi wa aina yoyote ile, hata huu wa simu kwa sababu inaonekana wakishapora tena wanaanza kutapeli watu.

"Masuala yote ya utapeli na uhalifu, mamlaka husika ni Jeshi la Polisi japo huwa tunapokea malalamiko kutoka kwa wateja na huwa tunawaelekeza sehemu husika kwa ajili ya hatua za kipolisi," alisema.

Hata hivyo, Nipashe ilipomtafuta Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, kwa kumwandikia maswali katika WhatsApp yake alisoma, lakini hakujibu na alipopigiwa hakupokea.

HABARI KITAIFA




Mitambo ya Kampuni ya Ujenzi ikisambaza lami katika ujenzi wa barabara ya Nyerere jijini Dar es Salaam jana.

# Mongella aeleza manufaa misaada na mikopo toka nje

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, John Mongella, amesema mikopo na misaada kutoka nje imechangia kasi ya maendeleo na kufanikisha miradi ya kiuchumi na kijamii katika sekta mbalimbali .

Amebainisha kuwa mikopo hiyo yenye masharti nafuu na misaada ya kifedha kutoka kwa mashirika ya kimataifa kama Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na nchi rafiki, imekuwa ikitumika katika kuboresha miundombinu, kuimarisha sekta za afya na elimu na kuchochea kilimo cha kisasa ambacho kinawanufaisha wakulima wadogo na kuongeza uzalishaji wa chakula.

Akizungumza na wanachama, viongozi wa chama katika halmashauri za Msalala na Kahama jana, Mongella alisema misaada hiyo pia imesaidia katika kuimarisha sekta ya afya kwa kununua vifaa tiba, kujenga hospitali na vituo vya afya, na kuboresha huduma za mama na mtoto.

Pia alisema misaada na mikopo hiyo imetumika katika kukuza ujuzi wa vijana kupitia mafunzo ya ufundi stadi, jambo ambalo limechangia kupunguza tatizo la ajira na kuongeza uzalishaji katika viwanda.

Kutokana na hali hiyo, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameonesha nia thabiti ya kuimarisha uchumi kupitia uwekezaji wa ndani nan je huku akiwajali wananchi wa kawaida na kuongeza kuwa dunia nzima sasa inatambua juhudi hizo ambazo shabaha yake kubwa ni kuleta maendeleo kwa wananchi.

Alisisitiza kuwa uongozi wa Rais Samia umekuwa wa kipekee, ukijikita katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na maisha yao yanaboreshwa kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Rais Samia ameonesha nia thabiti ya kuimarisha uchumi wa nchi kupitia uwekezaji wa ndani na nje, huku akiwajali zaidi wananchi wa kawaida. Pia serikali imeendelea kuboresha sekta mbalimbali kama afya, elimu, miundombinu na kilimo, ili kuhakikisha kila Mtanzania ananufaika na rasilimali za nchi," alisema.

Pia alisema jitihada za Rais Samia katika kuimarisha diplomasia ya kiuchumi zimesababisha Tanzania kupata fursa nyingi za kimataifa, ambazo zimechangia katika kukuza uchumi wa taifa.

Mongella ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Shinyanga alisema utawala wa Rais Samia umeonesha uwazi na uwajibikaji, hali iliyosaidia kujenga imani kwa wananchi na jumuiya ya kimataifa.

Vilevile, alisisitiza kuwa serikali imekuwa ikitekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kama vile ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), bwawa la umeme la Julius Nyerere, na kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama vijijini na mijini.

Kwa mujibu wa Mongella, juhudi hizo zimekuwa chachu ya maendeleo endelevu na zimevutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini.

Aliongeza kuwa Rais Samia amekuwa kiongozi mwenye maono, anayejitahidi kufanikisha malengo ya nchi katika kufikia uchumi wa kati na kuboresha maisha ya wananchi. Pia alisema ushirikiano wa kimataifa umeimarika chini ya uongozi wa Rais Samia, huku Tanzania ikijipatia heshima kubwa katika nyanja za kimataifa.

Katika hatua nyingine, Mongella alisisitiza umuhimu wa watendaji wa serikali na viongozi wa CCM kuiga mfano wa Rais Samia kwa kufanya kazi kwa bidii, uadilifu, na uwazi ili kuhakikisha malengo ya serikali yanafikiwa kwa ufanisi.

Mongella alizungumzia pia faida za uwekezaji katika sekta ya madini, hususan Kanda ya Ziwa, akibainisha kuwa ni moja ya maeneo ambayo yameleta tija kubwa kwa uchumi wa Tanzania.

Alisema kupitia uwekezaji huo, maeneo ya Kanda ya Ziwa yamenufaika kwa namna mbalimbali, ikiwamo ajira kwa wananchi wa kawaida, kuongezeka kwa mapato ya serikali kupitia kodi na kuboreshwa kwa huduma za kijamii kama elimu na afya.

Mkuu wa Wilaya ya Msalala, Mboni Mhita, alisema uwekezaji wa madini umechangia pia katika kuimarisha miundombinu ya eneo hilo, kwani barabara, huduma za maji, na umeme vimeboreshwa ili kusaidia shughuli za uchimbaji.

Alisema faida hizo si tu zimewanufaisha wakazi wa Kanda ya Ziwa, bali zimeongeza pato la taifa kwa ujumla, hali ambayo imechangia kupunguza umasikini na kuongeza ustawi wa jamii.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, alisema alisema serikali mkoani Shinyanga itaendelea kufanyia kazi kero za wananchi ili kufikia malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

## Majaliwa ataja mageuzi huduma watoto wachanga

**Na Halfan Chusi**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imefanya mageuzi makubwa kwa kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma kwa watoto wachanga.

Amesema serikali imekuwa ikitekeleza mikakati na afua mahsusi za kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa watoto wachanga.

Majaliwa amesema ni jambo la fahari kuwa hivi sasa huduma maalum za watoto wachanga na ile ya Mama Kangaroo hadi kufikia Julai 2024, zimeanzishwa katika hospitali 245.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi na wadau walioshiriki mbio za hisani za 2024 zilizoandaliwa na Benki ya Maendeleo (Maendeleo Bank Marathon 2024) katika viwanja vya Green Park, Oysterbay, jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu alisema mafanikio hayo yametokana na dhamira ya dhati ya serikali ya kuhakikisha Tanzania inapunguza vifo vya watoto wachanga kufikia lengo namba tatu la Maendeleo Endelevu la vifo chini ya 12 katika kila vizazi hai 1,000 kwa mwaka 2030 kutoka vifo 24 kwa kila vizazi hai 1,000 kwa mwaka 2022.

Kuhusu kaulimbiu ya tukio hilo ambayo ni Hatua ya Faraja - Msimu wa Pili, Waziri Mkuu alisema inasawiri mpango wa benki hiyo wa kuendeleza kazi yao ya mwaka jana ya ununuzi wa vitanda maalumu vya kutunzia watoto njiti (Infant Baby Warmer) katika Hospitali ya KCMC na ujenzi wa kituo kipya cha watoto wenye changamoto ya ulemavu wa akili na usonji kinachotarajiwa kujengwa wilayani Bagamoyo

"Kama mlivyosikia, pale KCMC, idadi ya vifo vya watoto wanaozaliwa njiti ni kubwa na ipo kati ya asilimia 20 mpaka 25. Hawa ni binadamu wenzetu wanaostahili kuishi na tuna kila sababu ya kuonesha upendo kwa kuchangia hatua za faraja.

"Hivyo basi, nitoe wito kwa wananchi wote wenye mapenzi mema kuendelea kuiunga mkono Benki ya Maendeleo katika utekelezaji wa afua hizi muhimu," alisisitiza.

Aidha, Majaliwa aliwapongeza viongozi wa benki hiyo kwa kuongeza lengo la uchangiaji kwenye mbio za mwaka huu kutoka Sh. milioni 120 hadi Sh. milioni 200, ili kukamilisha kazi waliyoianza mwaka jana

Kuhusu mchango wa madhehebu ya dini, Waziri Mkuu alisema serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa wadau wa sekta binafsi katika kutoa huduma za jamii zikiwepo zinazohusu sekta ya afya, elimu, maji na nyinginezo.

"Ninawapongeza sana Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania kwa kutoa eneo kubwa zaidi kwa ajili ya ujenzi wa kituo kipya cha watoto wenye changamoto ya ulemavu wa akili na usonji. Nimeelezwa kuwa kituo hicho kitajengwa eneo la Kitopeni, Wilayani Bagamoyo ili kukidhi mahitaji ya sasa ya jamii.

Aliwapongeza viongozi wa Benki ya Maendeleo kwa kufanikiwa kuongeza hadhi ya leseni ya uendeshaji kutoka kuwa Benki ya Kanda (Community Bank) na kupandishwa hadhi ya kuwa Benki ya Biashara ya Kitaifa (Fully-fledged Commercial Bank) kwani hatua hiyo inawaruhusu kufungua matawi nchi nzima.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vitendo hivi vya kuwatenga watu katika jamii katu visipewe nafasi

**WIKI** hii katika toleo mojawapo la gazeti la Nipashe, kulichapishwa taarifa kwamba katika vijiji vinne katika kata ya Kisiriri, Iramba mkoani Singida, umeibuka mtindo wa watu kutengwa na jamii iwapo watashindwa kulipa faini waliyotozwa kutokana na makosa mbalimbali wanayoyafanya.

Hatua hiyo ambayo imeibua mijadala katika jamii na taharuki kwa wananchi, imeanzishwa baada ya kuibuka kwa vikundi vya kimila, maarufu kama Nkiri. Vikundi hivyo vimeelezwa kuwatoza wananchi wanaofanya makosa kama vile kutoshiriki shughuli za kijamii faini kama vile ng'ombe, mbuzi au fedha. Yeyote anayetozwa faini hiyo kama inavyoamuliwa, anatengwa na jamii ikiwamo kutojumuishwa katika shughuli za kijamii.

Kwa mujibu wa uchunguzi wa Nipashe, vikundi hivyo vina safu za viongozi wanaosimamia utekelezaji wa mila au utamaduni huo na mwananchi asiyetoa faini hiyo, hutengwa na kijiji au kitongoji na haruhusiwi kwenda dukani kununua bidhaa yoyote.

Mwananchi anayeshindwa kulipa faini hiyo kama itakavyoamuriwa, haruhusiwi kwenda kusaga nafaka wala kwenda katika huduma za afya kupata matibabu na hawaruhusiwi kuhudhuria msiba utakapotokea katika eneo anamoishi na atakapofiwa hakuna atakayemfariji na atakayeonekana kafanya hivyo naye anatozwa faini.

Katika kuhakikisha yote hayo yanatekelezwa, vikundi hivyo ambavyo viko kila kijiji na kila kitongoji, vina sheria vilizojiwekea na wanufaika wakubwa wa faini hizo zinazotozwa ni pamoja na viongozi wa maeneo husika. Kuwapo kwa tatizo hilo kumekuwa kero kwa wananchi kwa kuwa hakuna hatua zozote kila wanapotoa taarifa kwa uongozi kutokana na kwamba ni sehemu ya wanufaika. Mbaya zaidi, vikundi hivyo vimekwenda hatua kubwa zaidi kwa kujiwekea mazingira ya kupata fedha au mifugo kwa faini kwa kuwatuhumu watu kuwa wachawi au wanasababisha vifo vya watu kimiujiza. Watu wanaodaiwa kufanya hivyo, wanatozwa hadi ng'ombe watatu na baadhi ya mifugo hiyo inayotozwa faini inachinjwa na nyama yake kugawiwa kwa wanakijiji wote au wanakitongoji.

Kwa mantiki hiyo, viongozi serikali na wa vikundi hivyo, wanapoona kuna uhitaji wa nyama au fedha, wanatengeneza mazingira ya kuwatuhumu watu kwa makosa na hatimaye kuwapangia faini hizo. Kwa kufanya hivyo, watu wanakamatwa na kudaiwa kuwa ni wachawi au wamehusika na vifo vya watu kwa njia za kishirikina na hatimaye kuwatoza fedha au mifugo. Jambo la kusikitisha ni kwamba wako baadhi ya wananchi wanaofikishwa katika vyombo vya sheria lakini wanaachiwa baada ya kubainika kuwa hakuna makosa ya kuwatia hatiani. Pamoja na kuachiwa na mahakama, viongozi hao wanang'ang'ania walipe faini vinginevyo watatengwa na jamii. Suala hili si geni katika jamii mbalimbali za Watanzania kwani limekuwa likifanyika miaka mingi katika mikoa mingi nchini lakini si kwa kumkomoa mtu au kikundi cha watu bali kuwafanya watu wawajibike ndani ya jamii wanayoishi. Mtu anaposhindwa kuhudhuria mkutano wa kitongoji, kijiji au msiba, anafikishwa katika baraza la kusomewa tuhuma zake kisha kumtoza faini iwapo atakiri au kutiwa hatiani kuwa ametenda kosa.


Pamoja na kuwapo huko, kwa namna linavyoendeshwa katika vijiji hivyo linavuka mipaka ya ubinadamu. Mtu atazuiwaje kupata huduma kama vile kununua mahitaji yake dukani au kupata matibabu katika kituo cha afya? Katika zama hizi za ustaarabu, jambo hilo halipaswi kupewa nafasi katika jamii ya Watanzania kwa sababu linarejesha hali ya kizamani ya ujima ambayo watu wanafikia hatua ya kukomoana. Jambo hilo linaweza kusababisha mauaji na hata ukosefu wa amani ndani ya jamii husika.

Wakati umefika sasa wa viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya wilaya hadi mkoa kuchukua hatua kwa kukemea kwa nguvu zote jambo hili pamoja na hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya wale wanaoendekeza tabia hizo. Hatua zinapaswa kuchukuliwa kwa sababu kama imefikia watu wanatuhumiwa kwa mauaji kwa njia za kishirikina, jambo hilo lisipokemewa linaweza kusababisha kushamiri na kuota mizizi kwa ramli chonganishi ambazo hatimaye zitafanya watu kuanza kuchukua sheria mkononi dhidi ya watuhumiwa. Mila na desturi zilizopitwa na wakati hazina budi kukemewa na kutokomezwa ili kuifanya jamii ya Watanzania, mahali popote, kuishi kwa amani, umoja na mshikamano badala ya uadui na uhasama. Vitendo kama hivyo havina nafasi na visipewe nafasi asilani.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni kwa manufaa yetu, tutoe maoni

Na Sabato Kasika

**KUTOA** maoni kunaweza kuwa na mchango wa kuboresha sera na mipango ya maendeleo ya nchi, hasa kwa kuzingatia mahitaji na matakwa ya wananchi. Hivyo, wananchi kushiriki katika kubuni na kutekeleza sera za maendeleo, ni jambo la muhimu.

Haki ya kutoa maoni ni ya msingi ya kila raia ambayo inalindwa chini ya Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Haki hii inahusu kila raia kutoa maoni ya kisiasa na kujieleza.

Ninagusia hilo ili kuzungumzia kidogo suala la Dira ya Taifa ya Maendeleo kwamba dira ni taswira na maono inayohusu mustakabali tarajiwa wa maendeleo ya nchi kwa miaka ya mbele.

Kwa sasa Tanzania iko katika mchakato wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Wananchi wanakaribishwa kutoa maoni yao kwa lengo la kuboresha dira hiyo kwa manufaa ya watu wake.

Njia mojawapo ya kuchukua hatua za kuchochea maendeleo, ni kila Mtanzania kushiriki, katika kutoa maoni ambayo yatasaidia kuifanya dira hiyo ifanye kazi kikamilifu.

Katika kufanikisha hilo, kwa sasa wananchi wanashirikishwa kwenye makongamano, semina na warsha ikiwa ni njia mojawapo ya kurahisisha ukusanyaji wa maoni yao.

Ni vyema wananchi wakajitokeza kwa wingi kutoa maoni, kwani hiyo ni sehemu ya upangaji maendeleo, ndio maana serikali imekuja na sera hiyo kama hatua madhubuti za kuchochea maendeleo ili kufikia kile ambacho nchi imekusudia katika mwaka huo.

Kwa njia hiyo ya kukusanya maoni ya wadau, ni wazi serikali imeweka mazingira rafiki kwa makundi mbalimbli ndani ya jamii ili kuyawezesha kutoa maoni ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Ni muhimu wananchi wakatambua kuwa wako huru kutoa maoni yao na mapendekezo ya jinsi gani ambavyo wanadhani serikali inaweza kufanya ili nchi ifikie maendeleo wanayoyataka.

Maoni ya wananchi yanaweza kuisaidia serikali kuangalia mafanikio ya mapungufu ya dira iliyopita na kuchukua hatua za kuiboresha ili kusonga mbele zaidi katika kuleta maendeleo.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inahusu maendeleo yetu, hivyo, kila Mtanzania hana budi kutambua umuhimu wake na kushiriki kutoa maoni, kwa ajili ya kuiboresha badala ya kujiweka pembeni.

Jambo la kuzingatia ni kwamba, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ni taswira na maono kuhusu mustakabali tarajiwa wa maendeleo ya nchi siku za usoni, hivyo, ni wajibu wetu kutoa maoni ya kuiboresha.

Maandalizi ya dira ni moja ya njia za upangaji maendeleo ya taifa ili liweze kustawi. Hivyo, wananchi ndio wachocheaji wa maendeleo kwa kutoa maoni ili kufikia kiwango tarajiwa katika siku za usoni.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko, kupitia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Tanzania imefanikiwa kupiga hatua kubwa ikiwamo kuingia kwenye orodha ya nchi ya uchumi wa kipato cha kati cha chini mwaka 2020 baada ya kufikisha wastani wa kipato cha mtu cha dola za kimarekani 1,080.

Ni muhimu wananchi kuendelea kushiriki katika kutoa maoni, hasa wakati huu wa maandalizi ya Dira 2050 kwa kuuangalia uhalisia ili kuuliza maswali ili kujua nini kimesababisha kufikia hatua hiyo na nini kifanyike ili kupiga hatua zaidi kwenye dira hiyo mpya.

Ninaamini kuwa kwa njia hiyo, itakuwa rahisi kujikwamua ili kufikia viwango vya juu vya kipato pamoja na ustawi wa maendeleo ya kila Mtanzania na taifa kwa ujumla.

Kwa sasa kuna baadhi ya vikundi ndani ya jamii ambavyo, vimeanza kuhamasisha wananchi kutoa maoni kuhusu dira hiyo, faida za kutoa maoni ili waweze kujitokeza kwa wingi kushiriki mchakato huo.

Miongoni mwa vikundi hivyo ni cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam, ambacho kimepanga kufikia watu 1,350 na kuwafundisha kutoa maoni, kwa njia ya simu ambayo baadaye yatachakatwa.

Watakaobahatika kufikiwa na kikundi hicho, ni vyema watumie nafasi hiyo vizuri kutoa maoni yao ambayo huenda yakawa na mchango mkubwa, katika uboreshaji wa dira kwa maendeleo ya baadaye.

MAKALA

FIKRA MBADALA

# Watanzania tuna matatizo ya kuendesha mambo yetu



Pascal Mayalla

KUMEPATIKANA habari njema kwenye ziara ya Rais Samia nchini China kwamba nchi hiyo imekubali kufanya ukarabati wa miundombinu ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na kuiendesha kwa faida.

Habari hizo ni njema kwa Watanzania na zinathibitisha China si tu mshirika mzuri wa Tanzania katika ujenzi wa miundombinu, bali pia ni rafiki wa kweli. Ni China ndiyo aliyojenga reli ya TAZARA ambayo inaanzia Dar es Salaam hadi Kapirimposhi nchini Zambia. Katika kufanya hivyo, hadi vibarua wote walitoka China na baada ya ujenzi, ukiondoa wale waliofia nchini na kuzikwa nchini, wengine wote waliondoka kurejea kwao.

Reli ya Kati ilijengwa na Mjerumani na vibarua walitoka India. Baada ya reli kukamilika vibarua hao walilowea Tanzania na ndio hawa wafanyabiashara wa jamii ya Waasia walipo ambao walijenga uhindini kila reli ilipopita kwenye miji mikuu yote.

Reli ya TAZARA ndiyo reli pekee ya Uhuru iliyojengwa baada ya Tanzania kupata uhuru. Kazi ngumu kabisa katika ujenzi wa reli, si kutandika mataruma bali ni kufanya upembuzi yakinifu na kuchanja njia ya kutandika hayo mataruma. Hata ujenzi wa kisasa ya SGR ambayo inajengwa sasa na imeshaanza kufanya kazi katika ya Dar es Salaam na Dodoma, upembuzi yakinifu na kuchanja au kuchonga njia ulikuwa ni mserereko wa reli ya kati kwa kupita mlemle kama tu kujaladia reli mpya kwenye njia ile ile ya reli ya kati.

Usafiri wa reli ndio wa gharama nafuu kabisa baada ya usafiri wa meli na reli ndio usafiri wenye uwezo wa kusafirisha abiria wengi na mizigo mingi kwa wakati mmoja na kwa gharama nafuu. Kati ya mipaka yote nchini Tanzania, mpaka wa Tunduma ndio mpaka unaongoza kwa kuwa biashara nyingi kutokana na malori ya mizigo inayokwenda Zambia kutokea bandari ya Dar es Salaam.

Reli ya TAZARA si tu ilisaidia sana kubeba mizigo ya Zambia na nchi jirani za Kusini mwa Tanzania, bali kuokoa barabara zetu na kupunguza msongomano mpaka wa Tunduma.

Kitendo cha reli ya TAZARA kulegalega, kumesababisha mizigo ya Zambia na nchi za kusini kusafirishwa kwa malori, hivyo kuharibu barabara, kuleta msongamano mpaka wa Tunduma, mizigo ya watu kuchelewa na ngarama za usafirishaji kuwa juu. Hali hiyo imisababisha jirani yetu Zambia kuamua kutumia bandari ya Msumbiji ambayo iko mbali zaidi, hivyo maboresho ya TAZARA ni habari njema sana kwa Tanzania.

Pamoja na kuwapo mpango huo, swali la kujiuliza, tulifikaje huko hadi TAZARA kushindwa kujiendesha kwa faida?. Na si TAZARA tu, hata bomba la mafuta la TAZAMA, kiwanda cha kusafisha mafuta cha Tipper, Shirika la Ndege Tanzania (ATC), reli ya kati, Kampuni ya Taifa ya Wakala wa Meli (NASACO) shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) Kampuni ya Mabasi ya Taifa (KAMATA) Bandari, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) na sasa Posta inachechemea.

Kama taifa, tumewahi kukaa chini na kutafakari tunakwama wapi? Nini kinachotukwamisha? Siku zote kisingizio kikubwa ni mtaji! Nimesema ni kisingizio tu kwa sababu kama ni mtaji, mbona tunakopa sana na serikali inatoa fedha nyingi kuyabeba mashirika yake na mfano mzuri ni ATCL imepewa ndege mpya za kutosha, mtaji mkubwa wa kutosha lakini bado inaendeshwa kwa hasara?

Hii reli ya SGR tunayoishangilia sana ruti ya DAR-Dodoma kupitia Morogoro, nayo kwak utegemea abiria tu, inaweza kusababisha hasara. Reli ya SGR haiwezi kujiendesha kwa faida kwa kubeba abiria. Ubebaji abiria kwenye SGR ni huduma tu bali faida ni kubeba mizigo mikubwa. Hayo yatapatikana baada ya kuanza kutolewa kwa huduma ya ubebaji wa mizigo kama ilivyobainishwa na uongozi wa TRC kuwa kukamilika kwake kutakuwa mkombozi katika kupunguza msongamano wa mizigo bandari ya Dar es Salaam.

Wakati wa serikali ya awamu ya nne chini ya Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete, wakipanga kujenga SGR pia walipanga ujenzi wa bandari ya Bagamoyo ili kuipatia SGR yetu mzigo wa kushiba. Mzigo unaopitia bandari ya Dar es Salaam, hauwezi kuishibisha SGR ikajiendesha kwa faida.

Hata uendeshaji wa reli ya kati, tuna matatizo. Faida kubwa ya bandari ya Dar es Salaam ni mizigo ya jirani zetu inayopita kwetu (transit goods). Tukajenga bandari kavu ya Isaka ili mizigo ya Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRCO, ikifika tu bandari ya Dar es Salaam, inapakiwa kwenye reli na kukimbizwa Isaka, malori ya Rwanda, Burundi na DRC yataikusanyia pale. Mara ya mwisho nimepita pale Isaka, hakuna kreni hata moja ya kushusha mizigo toka kwenye treni, hivyo hakuna mzigo unashushwa Isaka. Yale maghala ya TRC, yamekodishwa kwa Bakhresa.

Kwenye kikao kazi cha Ofisi ya Msajili wa Hazina na watendaji wakuu wa mashiriki ya umma, Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, aliyataja mashirika 40 ya umma ambayo ni mizigo, akapendekeza yafutwe. Huu ni uthibitisho sisi Watanzania tuna matatizo ya uendeshaji wa baadhi ya taasisi lakini zikibinafshishwa, zinashamiri. Hili tumelishuhudia kwenye Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) na Kampuni ya Sigara (TCC). Zilipokuwa chini ya serikali zilikuwa hoi bin taabani lakini baada ya kubinafsishwa mambo yakaanza kuwa mazuri.

Wakati wa kelele za ubinafsishaji wa bandari, tulishauri, kitu cha kwanza kwa sisi Watanzania, ni kujitathmini tunakwama wapi? Tukijigundua tuna matatizo ya uendeshaji wa baadhi ya miradi, kwanza tukubali makosa, kisha tutafute ufumbuzi. Ikitokea ufumbuzi wa baadhi ya matatizo yetu yatahitaji kusaidiwa, hakuna ubaya kuomba msaada. Kuna nchi zinasaidiwa kuendesha baadhi ya miradi na sasa kwa kadiri dunia inavyobadilika kidigitali, utafika wakati tunaweza hata kujikuta tukaikodisha Ikulu yetu kwa mwekezaji kuiendesha kwa faida!

Kwenye hili la kuikodisha Ikulu yetu kwa mwekezaji atuendeshee, mnaweza kudhani ninatania! Mwenzenu nimebahatika kufika ikulu mbalimbalimbali za wenzetu duniani zikiwamo Afrika Kusini, White House, St. Peters Basilica pale Roma, Buckemham Palace Uingereza. Ikulu ni eneo la kivutio cha watalii, mfano mdogo ni angalia jengo la Beit Al Ajab Zanzibar. Enzi za uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere, Ali Hassan Mwinyi na Benjamin Mkapa tulikuwa tunapita kule nyuma ya Ikulu kwenda Feri. Enzi za JK kukafungwa eti kwa sababu za kiusalama!, JPM alipoingia amepapendezesha Ikulu kwa kujaza wanyama na kuzalisha tausi, yote haya ni ya nini kama Ikulu inafungwa?

**Wasalaam. Paskali**
**+255 754 270403**

# Manyoni yaongoza migongano wanyama, binadamu

**Na Joseph Mwendapole**

WAKATI matukio ya migongano baina ya binadamu na wanyamapori yakiendelea kuongezeka nchini, wilaya ya Manyoni mkoani Singida, imetajwa kuongoza kwa matukio hayo.

Ofisa Mhifadhi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), Isaac Chamba, aliyasema hayo jana Bagamoyo, mkoani Pwani, wakati akitoa mada kuhusu namna mamlaka inavyopambana na migongano baina ya binadamu na wanyama hao.

Alikuwa akizungumza katika kongamano la siku mbili lililoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) kwa waharíri wa vyombo mbalimbali vya habari.

Kongamano hilo linajadili mradi unaotekelezwa na serikali wa kukabiliana na migongano ya binadamu na wanyamapori, unaofadhiliwa na Wizara ya Kiuchumi ya Maendeleo kupitia Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ).

Chamba alisema matukio ya migongano baina ya binadamu na wanyama kwa mwaka 2018 yalikuwa 997 na mwaka 2023 yameongezeka hadi kufikia matukio 3,496, yakihusisha uvamizi wa tembo.

Alisema takwimu za mwaka 2023/24, zinaonesha kuwa Wilaya ya Manyoni, ilikuwa na matukio 410, Nachingwea 312, Lindi 260, Tunduru 218, Busega 214, Rufiji 202, Bunda 158, Liwale 112 na Chamwino matukio 111.

Alisema tembo amekuwa akichangia kwa asilimia 80 katika migogoro hiyo, akifuatiwa na Simba asilimia sita, Kiboko asilimia tano, Kifaru asilimia nne, mamba asilimia tatu na Fisi asilimia mbili.

Chamba alitaja baadhi ya sababu za migongano hiyo ni uharibifu wa njia za asili za wanyamapori (shoroba), zilizovamiwa na wananchi kufanya makazi na shughuli za kilimo na ufugaji.

Alisema sababu nyingine ni kukosekana kwa mpango bora wa matumizi ya ardhi ambapo baadhi ya wananchi wamejikuta wakivamia na kuishi maeneo ya hifadhi.

"Kuna wakati mifugo ya kawaida inavamia hifadhini, sasa kwa mazingira ya kawaida wanyamapori hawapatani na hawa wanaofugwa wengine wamefungwa kengele au kupuliziwa dawa za aina mbalimbali.

"Kwa hiyo wanyamapori wanapokutana na mazingira hayo ya harufu ya dawa au kelele za kengele, wanaona ni kero kwao kwa hivyo, wanahama maeneo yao na wanajikuta wamehamia katika maeneo yenye makazi ya watu na hapo ndipo migongano inaapoanza," alisema.

Chamba alitaja sababu nyingine kuwa ni mabadiliko ya tabia nchi kama kuwapo kwa ukame mkali au mafuriko, kunakosababisha wanyama kuhama kutoka maeneo yao ya asili kwenda kutafuta mawindo.

"Kama mnakumbuka mafuriko ya Rufiji yaliyotokea mwaka jana, yalisababisha mamba kusambaa kutoka maeneo yao na kwenda kwa wananchi na kusababisha taharuki," alisema.

Alitaja sababu nyingine ni baadhi ya wananchi kupuuza ushauri wa wataalam kuhusu namna ya kujilinda wanapowaona wanyamapori katika maeneo yao.

"Kuna tukio la mwaka juzi, lililotokea mkoani Mtwara, mwalimu alijipiga picha na tembo. Yule tembo alishikwa na hasira akamvuta, akamkanyaga na kumuua. Hatukutarajia mtu wa kiwango cha mwalimu kufanya tukio la hatari na kujisababishia madhara aliyopata," alisema.

Chamba alisema pia, imani potofu imekuwa ikichangia kwa baadhi ya makabila, kutumia wanyama wakali kama fisi kama chombo cha usafiri na chombo cha kufanyia mawindo katika maeneo yao.

"Kuna makabila baadhi ya watu wanafuga fisi katikae makazi yao na wakati mwingine wanavamia na kuua mifugo ya wananchi wengine na kusababisha migogoro na wenye mifugo,"

# Zungu awashusha wabunge presha majimboni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Spika wa Bunge, Mussa Zungu amewatoa hofu wabunge wasiogope kurudi majimboni na kuwataka kujipanga maneno ya kuwaambia wananchi wao kwa kuwa wanazo sifa za kurudi bungeni 2025.

Akizungumza wakati wa kuahirisha bunge jana, Zungu aliwapongeza wabunge kwa kazi nzuri waliyofanya kipindi chote ambacho wapo bungeni, na wameonesha umahiri na wana sifa za kurudi tena ubunge 2025.

"Mnayo maneno ya kusema jimboni, msiogope. Msiogope wajumbe, msiogope wagombea, mnayo maneno ya kusema msirudi na unyonge nendeni mkasifie serikali ya Mama Samia na neno la mwisho ukiishi mbinguni usiogope radi."

"Niwaombe msiogope kwenda majimboni, nendeni majimboni hiki ni kipindi cha kwenda kuzungumzia faida ambayo tumeipata kutokana na uongozi mahiri wa Rais Samia Suluhu Hassan kuna miradi ya kutosha ya kuzungumzia hata juzi Rais amesaini mradi wa kuendeleza biashara na reli yetu ya TAZARA,"alisema.

Alisema hatua hiyo inatokana na kiwango kikubwa cha ufanisi wa diplomasia.

# Programu imarisha uchumi kuwainua, kuwatoa wajasiriamali kimasomaso

**Mussa Mwangoka,** MPANDA

BARAZA la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limesema Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia, ni chachu ya kuleta mapinduzi ya kiuchumi kwa wajasiriamali wa mkoa wa Katavi, kupitia vikundi vya wanawake, vijana na makundi maalumu.

Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng` Issa, alisema hayo juzi wakati wa mafunzo elekezi kuhusu utekelezaji wa programu hiyo kwa viongozi wa mkoa yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa mkoa mjini hapa.

Alisema baraza kupitia programu hiyo, limedhamiria kuwakwamua kiuchumi wajasiriamali hao kwa kuwawezesha ujuzi na mitaji ya shughuli zao za ujasiriamali.

Alisema NEEC inatambua kuwa mkoa wa Katavi una fursa nyingi za kiuchumi katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara ya kusindika mazao, hivyo kupitia programu hiyo, wananchi watajikwamua kiuchumi kupitia vikundi vyao.

Issa alisema baraza limejipanga kuwaunganisha wanawake na makundi mengine na taasisi mbalimbali likiwamo Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kupata technolojia na vibali mbalimbali.

Pia aliwataka wajasiriamali kuwa na nidhamu ya fedha kwa kuweka katika akaunti au vibubu ili kuendeleza biashara zao.

Issa alisema programu hiyo ina jukumu la kuwaunganisha wanawake hapa nchini na fursa zilizopo.

"Moja ya jukumu letu ni kuhakikisha pamoja na sera ya serikali ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, ni muhimu kuhakikisha tunawaunganisha wanawake kwenye shughuli zote za uchumi na miradi ya kimkakati nchini," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, alisema ni matumaini yake kwamba kupitia programu ya IMASA, mkoa wa Katavi utapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya utapiamlo na udumavu.

"Pamoja na kwamba tumeshuka kutoka 38 hadi 32 katika mikoa inayoongoza kwa utapiamlo nchini, kupitia programu hii changamoto ya utapiamlo itatafutiwa ufumbuzi kwani elimu ya lishe bora itatolewa kwa wananchi na bahati nzuri mkoa huu unazalisha chakula kwa wingi," alisema.

Mmoja wa wajasiriamali, Hellen Nondo, kutoka kikundi wa wauzaji wa matunda na mboga, alisema changamoto kubwa inayowakabili ni ukosefu wa mitaji kwa ajili ya kupanua wigo wa biashara, hivyo wanahitaji kupata mikopo ili kukuza mitaji hiyo.



Mashimo yaliyochimbwa katika eneo la Hospitali ya Wilaya ya Kivule jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujenga Uzio wa eneo hilo yakiwa yameachwa kwa muda mrefu bila kujengwa na kuleta usumbufu kwa wananchi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yawatoa hofu walioandikishwa katika daftari la mpigakura kuanzia 2015

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewatoa hofu wananchi walioandikishwa kupiga kura mwaka 2015 na mwaka 2019/20 kuwa kadi zao ni halali na zitatumika katika Uchaguzi Mkuu, 2025.

Imesema uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura halihusishi kubadilisha kadi za wapigakura zenye jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kupata kadi iliyoandikwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Akitoa juzi hoja ya kuahirishwa Bunge hadi Oktoba 29, mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema kwa kuzingatia maboresho hayo, kadi za wananchi hao ni halali.

Majaliwa alisema kadi hizo ni halali kwa mujibu wa kifungu cha 168 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani namba moja ya Mwaka 2024 na zitatumika katika Uchaguzi Mkuu.

Alisema kwa mujibu wa kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani namba moja ya mwaka 2024, uboreshaji huo unahusisha watanzania wote wenye sifa za kuandikishwa wenye umri wa miaka 18 au zaidi na wale watakaotimiza umri huo wakati wa uchaguzi mkuu.

Pia alisema uboreshaji wa daftari unatoa fursa kwa wapiga kura walioandikishwa na kwa bahati mbaya kadi zao zimepotea au kuharibika na wale ambao wamehama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda jingine, ama kuhamisha taarifa zao kufika vituoni ili kupata kadi mpya.

Alisisitiza kuwa wadau wa ngazi ya taifa, mkoa na halmashauri, wahakikishe wanavishirikisha vyama vya siasa katika mchakato huo kwa kuwa wao ni wadau muhimu katika masuala ya uchaguzi.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, Majaliwa alisema maandalizi mengine ya uchaguzi yapo katika hatua za ukamilishaji ambayo yanajumuisha kutangaza orodha ya maeneo ya utawala, uhakiki wa vituo vya kupigia kura awamu ya pili na manunuzi ya vifaa vya uchaguzi.

Aliwaomba wabunge na wadau wengine kuhamasisha wananchi kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, huku akisisitiza watanzania wote kuwa tayari kutimiza haki yao ya kikatiba kwa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu.

Katika hatua nyingine, Majaliwa alisema serikali imeendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato nchini ambapo hali ya ukusanyaji wa mapato ya ndani katik mamlaka za serikali za mitaa katika kipindi cha mwezi Julai, 2024, kuendelea kuimarika.

"Jumla ya Sh. bilioni 113.701 kimekusanywasawa na asilimia nane ya makisio ya mwaka 2024/2025 ya Sh. trilioni 1.356. Aidha, makusanyo halisi yameongezeka kutoka Sh. bilioni 90.665 yaliyokusanywa kipindi kama hicho cha Julai, 2023 ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 23.036," alisema.

Majaliwa alisema ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya ndani katika mamlaka za serikali za Mitaa, linachangiwa na mikakati mbalimbali inayoendelea kufanywa na serikali ambayo ni usimamizi wa vyanzo vya mapato vilivyoko, zoezi la mara kwa mara la ufanyaji tathmini ya vyanzo vya mapato ya ndani ya kila halmashauri kwa halmashauri zote 184.

Pia alisema mkakati mwingine ni kutoa elimu ya ulipaji ushuru kwa wananchi, pamoja na kuendelea kusimimamia matumizi sahihi ya Mfumo wa TAUSI wa ukusanyaji mapato pamoja na mashine za kukusanyia mapato (POS).

MAISHA
SEPTEMBA 8, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana



ROSTI YA KABEJI
Ukurasa 14





# BUTI USIICHUKULIE POA

Ukurasa 13

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| O | ■ | J | E | M | B | E |
| N | ■ | ■ | ■ | K | ■ | N |
| G | ■ | F | A | O | ■ | D |
| O | V | U | ■ | S | I | E |
| Z | ■ | M | O | I | ■ | L |
| W | ■ | B | ■ | ■ | ■ | E |
| A | M | A | N | A | ■ | A |

## FUMBO TOTO

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


ARA, DAU, MBU, TIN, OTANA, FUNDA, NINDU, TAMKA, AMBULIA, MAKALIO

## AMSHA AKILI


JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 4 | 2 | 3 | |
| 1 | | 2 | 4 |
| | | | |


## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake “usiku mwema mwanangu”

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao “Pata njozi njema mwanetu”

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuaambia “usiku mwema mpendwa wetu”

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia “Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani”

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Athari za kumwacha mke wa kwanza

KARIBU tena masomaji wangu katika mwendelezo wa mambo yanayotikisa familia zetu katika masuala ya ndoa. Yako mengi watu wanapitia kwenye nyumba zao wanakaa kimya lakini mwisho wa siku hujidhihirisha hadharani.

Wako watu wamekuwa wakioa na kuachana jambo ambalo linaonekana kama ni fasheni, ni kawaida tu ya kimaisha. Mungu anachukia watu kuachana na anasisitiza mwanaume amfurahie mke wa ujana wake.

Lakini je, hili linatekelezwa? Neno la Mungu katika Biblia Takatifu linasema: "Maana BWANA amekuita mke aliyeachwa na kuhuzunishwa rohoni, kama mke wakati wa ujana, atupwapo, asema Mungu wako." (Isaya 54: 6)

Usimtende mke wa ujana wako mambo ya hiana kwani huyo ni mwenzako, na mke wa agano lako. "Hakuna mtu mmoja aliyetenda hivi; ambaye alikuwa na ufahamu kidogo.

"Au je! Kuna mtu mmoja atafutaye mzao mwenye kumcha Mungu? Kwa hiyo, jihadharini roho zenu; mtu awaye yote asimtende mke wa ujana wake mambo ya hiana." (Malaki 2: 15)

Msomaji wangu, Mungu alishatoa tahadhari mapema kuhusu mke wa ujana wa mtu. Lakini wapo waliopuuza wakajikuta katika wakati mgumu sana. Hebu sikia mfano wa familia hii.

Yuko baba mmoja alikuwa na familia nzuri mke na watoto wake kadhaa. Alikuwa pia na kazi ofisi za serikali na alipendwa na wengi hasa kutokana na ucheshi wake.

Akafikia hatua akajisahau akatafuta mahusiano nje ya ndoa yake. Akakutana na mwanamke mmoja aliyekuwa na watoto wake watatu. Mama huyu ni mamalishe, hupika vyakula na wateja wanavutiwa sana na mapishi yake.

Kumbe anatumia nguvu za giza kuvuta wateja. Baba yule akanaswa akawa habanduki akamfanya kuwa mke wa pili (dini inamruhusu).

Tatizo likawa kwamba hakumbuki tena kumhudumia bi-mkubwa kwani mahaba yote yaligeukia kwa bi-mdogo ambaye watoto wake alizaa na wanaume tofauti. Baba huyu akaamua kutoa matunzo yote hadi kuwasomesha.

Kwa bi-mkubwa anarudi lakini mkali, dharau na wala fedha za matumizi haachi. Mama akaamua kuanzisha biashara ya kupika vitumbua ili mkono uweze kwenda kinywani. Akawa pia anawategemea wanawe ambao nao hawana mtaji mkubwa lakini angalau walimletea chochote maisha yaendelee.

Mama akila dagaa, bi-mdogo ananunuliwa nyama kilo moja karibia kila siku. Bi-mkubwa akawa anamshukuru Mungu kwa chochote anachomtakabali.

Awali nimeonesha jinsi Mungu anavyotoa tahadhari kuhusu kumfanyia hiana mke wa ujana wako. Nini kilichotokea kwa baba huyu niliyemjadili hapo juu?

Hivi sasa anatia huruma. Baba aliamka siku mmoja akapatwa na kiharusi, upande mmoja haufanyi kazi kuanzia mkono na mguu. Hivyo, hawezi tena kwenda kazini. Yule bi-mdogo akamwagiza aende kwa mjomba wake mkoani akamtibu kwani ni mganga wa kienyeji.

Pamoja na jitihada hizo, bado hajakaa sawa anajitahidi kutembea na fimbo lakini ndio hawezi tena kufanya kazi yoyote. Anaweza kutoka nyumbani asubuhi anaenda kwa watu aliowajua awali wamsaidie kama siyo fedha angalau wampe chakula, kisha anarudi kwa mke mkubwa.

Mungu anasema: "Mtu awaye yote asimtende mke wa ujana wake mambo ya hiana." Matokeo yake ndiyo kama haya yanayomsibu baba huyu. Bila shaka anajutia aliyomfanyia mke na kumuegemea mke wa kando.

Alimdharau mke wa ujana lakini amerudi kwa aibu, lakini sasa mke amfanyie nini? Wakati akiwa na uwezo na kazi nzuri angempa mtaji akaanzisha mradi wa familia ingekuwa baraka sana. Lakini baba huyu aliwekeza kwa bi-mdogo ambako wala hawezi kukaa.

> **Lakini je, hili linatekelezwa? Neno la Mungu katika Biblia Takatifu linasema: "Maana BWANA amekuita mke aliyeachwa na kuhuzunishwa rohoni, kama mke wakati wa ujana, atupwapo, asema Mungu wako." (Isaya 54: 6)**

Wako kina baba wengi wameziasi nyumba zao kwa sababu mbalimbali na kuanzisha mahusiano kwingineko. Lakini baadhi yao wameanguka kimaisha kwa kuivunja ile kanuni ya Mungu ya kutomuacha mke wa ujana wako! "...yeye ni mwenzako, mke wa agano lako" (Malaki 2:14).

Wengine waliwafukuza kabisa wake zao ambao nao walikwenda kupata wanaume wengine waliowapa utulivu. Lakini wao (wanaume) wakajikuta wanayumba na pengine kuteswa na hao nyumba ndogo. Chanzo ni kuwaacha wake zao kwa hiana, jambo ambalo Mungu alitoa tahadhari mapema kwenye mausia yake.

Msomaji wangu, kumbuka kile unachokipanda leo ndicho utakachovuna kesho yako. Unamtenda mtu jambo jema yeye anakulipa kwa baya? Huyu hawezi kubaki salama. Wewe tenda wema uende zako, usingoje shukrani!

***Je, una maoni au kisa? Ujumbe mfupi 0715268581***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Serikali ituambie ni vikundi vingapi vimekufa?

JULAI Mosi, mwaka huu, serikali ilianza kutoa tena pesa za mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na mamlaka za serikali za mitaa, kwa maana ya halmashauri, baada ya kusitishwa Bungeni Dodoma Aprili 13, 2023.

Ninafahamu kuwa uandaaji wa kanuni, mwongozo, vitini vya mafunzo na maboresho ya mfumo wa kielektroniki wa utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi umekamilika.

Bila kificho, Mkurugenzi wa Tawala za Mikoa, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Beatrice Kimoleta, ameeleza kwamba wamefanya mambo mbalimbali kuboresha mikopo hiyo kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha, mapitio ya kanuni za mikopo, uandaaji wa miongozo na vitini vya mafunzo.

Katika kipindi chote ambacho mikopo hiyo ya makundi maalum ya wanawake, vijana na wenye ulemavu ilikuwa imesitishwa, halmashauri zilitenga fedha hizo lakini marejesho kwa vikundi vilivyokuwa vikidaiwa yalikuwa yanaendelea, hivyo fedha zipo za kutosha.

Swali la kujiuliza hapa, kwa wakati wote huo wa utekelezaji wa sera hiyo, ni vikundi vingapi vilipata fedha hizo na kufa rasmi? Mbona hatuambiwi na ni suala la kisera?

Hata hivyo Aprili 16, mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, alitangaza kurejeshwa kwa mikopo hiyo wakati akisoma makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2024/25.

Alisema halmashauri 10 za majaribio zitaanza utoaji wa mikopo hiyo kwa kutumia benki.

Kwa mujibu wa Waziri Mchengerwa, mikopo inayotolewa ni Sh. bilioni 227.96 huku Sh. bilioni 63.67 zikiwa fedha za marejesho zilizokuwa zikiendelea kukusanywa kutokana na mikopo iliyotolewa kabla ya kusimamishwa.

Mchengerwa alisema Sh. bilioni 63.24 ni fedha zilizokuwa zinatengwa kwa ajili ya mikopo na Sh. bilioni 101.05 ni zile zilizotengwa kutokana na makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya mwaka 2024/25.

Anyway! Wiki hii nimemsikia Mwanaharakati na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Jamii la Tusonge CDO, Aginatha Rutazaa, akisema vikundi vingi vya wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 vinavyohusisha makundi hayo vinakufa kwa sababu vinapoingia kwenye muunganiko, maslahi binafsi yanatawala zaidi na kumeza maslahi ya kikundi.

Kwamba, matokeo yake kikundi hicho hudhoofika na kufa na viongozi kuwa wa kwanza kupeleka jeneza kwenye kaburi, kuzika kukundi ambacho wenyewe wamejiita ni viongozi.

Anasema chanzo kikubwa cha kufa vikundi vingi, ni matumizi ya hovyo na wanachama kukosa nidhamu ya fedha.

Akaenda mbali zaidi akisema, ukichunguza matumizi ya siku ya wanachama wengi, ni matumizi ya hovyo.

Eti mgeni amekuja nyumbani kwake anakimbilia kumwuliza unakunywa soda gani? Kwani mgeni kakwambia umnunulie soda? Kwa nini unaingia kwenye matumizi yasiyo sahihi?

Akasema nidhamu ya fedha ni pamoja na kujizuia kufanya vitu ambavyo ukiviangalia mbele havina matokeo, sio kukufaidisha tu wewe, matokeo ya kufaidisha pia familia yako na jamii kwa wigo wake.

Namnukuu: "Nidhamu ya fedha ni kitu muhimu na ndio siri ya mafanikio. Watu waliojenga maghorofa, wenye kampuni kubwa, wenye maisha ya kufuru, ni watu walioanza na mtaji wa Sh. 10,000 hadi 20,000, wauza karanga, wapiga viatu rangi waliokuwa na nidhamu ya fedha.

"Leo hii wenye kampuni kubwa walioajiri watu na wanaoweza kupata kipato kikubwa ambacho kinasaidia serikali yetu na kusaidia ustawi wa Tanzania. Ukiiambia serikali kwamba, kuna kikundi cha wanawake na wanaume 30 wanaouza nyanya, mboga na vitunguu cha Amkeni Vicoba Group katika Manispaa ya Moshi, wamejikusanya wao wenyewe, na akaunti yao inasoma shilingi milioni 62.5 watashangaa."

Ni hivi! kikundi chenye mafanikio makubwa kiuchumi, kinachochoea uungwaji mkono makundi maalum ya jamii yanayonufaika na sera ya serikali ya mikopo isiyo na riba

Mara nyingi vikundi kama hivi vimeundwa, lakini vinakufa mwaka unaofuata kwa sababu vinakuwa ni nguvu ya soda, na vinaishia kuteketea kama moto wa magunzi.

Vikundi vyote vinavyofanikiwa, ni vile ambavyo wanachama wake wamekana nafsi zao, na wakaweka hisia zao na maslahi yao binafsi pembeni; wakaweka mbele maslahi ya pamoja.

**• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HONGERA MC GARAB





Ilikuwa siku ya kukumbukwa kwa muongozaji sherehe mbalimbali Mc Garab baada ya kufurahia kumbukizi ya siku yake ya kuzaliwa wiki hii. PICHA: MC GARAB





# MITINDO

Na Moshi Lusonzo





## BUTI USIICHUKULIE POA

BUTI ni aina ya kiatu kikubwa kinachofunika mguu na wakati mwingine hadi kwenye goti.

Mara nyingi buti hutengenezwa kwa ngozi, lakini zipo zinazotumia malighafi ya plastiki.

Kwa kawaida viatu vya aina hii huvaliwa na watu maalumu kama vikosi vya jeshi au kazi ngumu.

Kulingana na wabunifu wake, buti huvaliwa kwa kazi maalumu ili kulinda mguu kutokana na maji, baridi kali, matope au hatari ya kemikali au mafuta.

Buti za kwanza hazikuwa zimeundwa kama zile za leo ambazo zinaweza kuvaliwa na kila mtu, ilikuwa na kifaa cha kukanyagia pamoja na kitambaa kinachofunika mguu hadi juu ya goti.

Hata hivyo kuanzia miaka ya 1000 KK, buti zilipata sura mpya huku waundaji wakitumia ngozi kutengeneza.


Lakini kila miaka inavyozidi kusonga mbele watengenezaji wamebuni buti za aina mbalimbali ambazo hutumiwa na watu wote na kuwa miongoni mwa viatu vinavyopendwa duniani.

Katika majukuwaa ya mavazi, kumekuwa na maonesho ya viatu vya aina hii katika mitindo mbalimbali ya kupendeza na kusababisha vijana kuchangamkia.


Kwa mfano viatu vya buti huvaliwa na watu mashuhuri kama wanamuziki, wacheza filamu, wanamichezo na wanafamilia za kifalme.

UREMBO

Na Mary Geofrey







# Ng'arisha uso kwa 'Make Up'

VIPODOZI au wengine wanafahamu kama Make Up ni urembo unaopendwa kutumiwa na wanawake wengi kwa lengo la kubadili mwonekano wa sura ili kuongeza uzuri.

Wale wanaopenda kujiremba wenyewe nyumbani kuna mambo muhimu tunakumbushana ili kuyazingatia kabla ya kutumia vipodozi.

Jambo kubwa kabisa tafuta vipodozi vinavyoendana na ngozi yako, usinunue au kupaka kwa kufuata mkumbo.

Kumbuka kila mtu ana rangi yake ya ngozi, mfano poda zimetengenezwa na aina mbalimbali za rangi.

Hivyo, inakupasa kufanya utafiti ili kubaini unapata vipodozi sahihi na havina madhara katika ngozi yako.

Watu wenye ngozi za mafuta wanashauriwa kupaka vipodozi vya jamii ya poda au ungaunga kwani cream inaweza kuziba matundu ya hewa usoni na kusababisha chunusi.

Wale walio na ngozi kavu fahamu kuwa, vipodozi aina ya cream havina uwezo wa kukaa muda mrefu katika ngozi, hivyo ikiwa unahitaji kuonekana mrembo kwa muda usiopungua saa nane ni vyema ukapaka poda.

Jambo jingine la kutilia msisitizo ni namna ya kupaka aina zote mbili za vipodozi, inashauriwa poda ipakwe kwa brashi zake maalumu, siyo mikono wala kitambaa chochote ambacho hakijawekwa mahususi kwa kazi hiyo.

Ila kwa upande wa cream au majimaji, inapaswa kupakwa kwa mikono na kusambazwa katika uso wote, ili kuwe na ulinganifu katika eneo hili linalokusudiwa.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Rosti ya kabeji

KABEJI ni mboga yenye virutubisho vizuri kwa ajili ya afya ya binadamu ikiwamo Vitamin. Wengi hawapendi mboga hii kwa sababu mbalimbali lakini nakuhakikishia kwa mapishi haya ya rosti utaipenda.

**Mahitaji**

Nyama, chumvi, tangawizi, kitunguu saumu punje moja kile kikubwa, limao, kabeji, nyanya ya kopo ya kawaida, kitunguu maji, mafuta ya kupikia, karoti na pilipili hoho. Mahitaji yako yataendana na kiasi cha mboga unayopika.

**Namna ya kuandaa**

Andaa vitu vyote kwa kuvikatakata vizuri, weka chombo cha kupikia jikoni kisha uweke mafuta ya kupikia kiasi. Walau vijiko vitatu vya chakula yakipata moto weka nyama yako na anza kukoroga.

Acha nyama ijikaange kwa dakika 3, kisha weka kitunguu maji. Baada ya sekunde kadhaa ongeza hoho na karoti na ukamulie limao katika mchanganyiko huo.



Usitumie limao zima kwa sababu nyanya ya pakti ina uchachu hivyo utaharibu mboga yako. Subiri kwa sekunde 30, kisha weka robo ya nyanya ya pakti, ikishajikaanga na mchanganyiko ongeza nyanya za kawaida na chumvi kiasi upendacho kisha funika ili mchanganyiko wako uive mapema.

Nyanya zitakapokaribia kuiva, weka kabeji na uichanganye vizuri na mchanganyiko kisha ongeza pilipili na uache pishi lako lichemke kwa dakika 5 hadi 7.

Onja chakula na kama kabeji haijaiva, weka maji kidogo ili iive haraka. Usiongeze maji mengi kwani itafanya kabeji yako iive sana na kuharibu virutubisho.

Hadi hapo, mboga yako itakuwa tayari. Kama unataka kula na iko tayari na ugali utanogesha zaidi mlo wako.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya





# Ujenzi wa nyumba uwekezaji wa maana

UJENZI wa nyumba ni uwekezaji kama ulivyo uwekezaji mwingine wowote. Ni vigumu sana kufanikisha kuwa na nyumba ya ndoto yako endapo hujaweka mipango mizuri ya kuweka pesa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hiyo unayoitamani.

Mtu anapojenga nyumba ya kupangisha kwa ajili ya makazi au biashara, anajiweka katika nafasi nzuri ya kujiongezea kipato na kukuza uchumi wake na familia kwa ujumla. Hata hivyo, kabla ya kufanya hivyo, mtu anayewekeza katika ujenzi wa nyumba anapaswa kuyajua mambo kadhaa.

Mtaalamu wa ujenzi Khamis Ally anasema vipo vitu ambavyo mtu ambaye amekusudia kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba anapaswa kuvifahamu.

Mojawapo ya vitu hivyo, anasema ni kuweka mipango madhubuti juu ya ujenzi wa nyumba katika mtazamo wa sasa na baadae.

"Unapopanga kujenga nyumba yako ni muhimu kuiona baadae na mabadiliko yake, ni vema ujue jengo lako litakavyokuwa kabla ya kuanza ujenzi, ufahamu uzuri wake, ukubwa, kimo na rangi.

"Ujue ni wapi utakwenda kununua saruji, mbao, nondo na vinginevyo, umfahamu fundi atakayekujengea, ukanda unaojenga ni wa aina gani kijiografia, ufahamu kama eneo lako halina mgogoro wowote iwe ni kwa upande wa serikali au majirani," anasema.

Jambo lingine ambalo mtaalamu huyu anashauri ni kujenga nyumba inayokidhi mahitaji yako. Anasema ni muhimu kufahamu ni nyumba ya aina gani unayotaka kujenga kwa kutazama mahitaji yako katika uhalisia wa sasa na wa baadae na kumshirikisha mtaalamu aliyebobea katika usanifu wa nyumba za kuishi.

"Kujenga kwa kuzidi mahitaji yako, inaweza leta hasara ya kushindwa kumaliza ujenzi. Unaweza ukajiuliza maswali kadhaa, Je, kuishi kwenye hiyo nyumba ni faida zaidi kuliko kupanga?,Ni muhimu kuhakikisha kwamba unajenga kwa faida na si hasara.

"Baadhi wamejikuta wamejenga nyumba ambayo inadumu kwa muda mfupi, wapo waliofikiri kutumia vifaa duni vyenye gharama ndogo ndio namna ya kupunguza gharama na badala yake walijikuta wakihitajika kuvibadili baada ya muda mfupi na kwa gharama kubwa zaidi.

"Wako pia waliochakachua kwa kujua kwamba ndio njia nzuri ya kupunguza gharama, na kujikuta katika hatari za nyufa, kubomoka na kutokudumu kwa muda unaofaa. Hakikisha unakuwa na mtazamo wa kiuchumi wa kujenga kilicho bora, imara, kinachodumu na kwa gharama nafuu," anasisitiza.

Ally anasema kwamba kabla ya kuanza ujenzi wa nyumba yako, ni vizuri pia ukadodosa na kupata taarifa sahihi zinazohusiana na ujenzi ikiwamo gharama ambazo hutumika kulipa mafundi, vifaa vinavyopaswa kununuliwa ili kukusaidia kufanya uamuzi bila hofu na usionekane hujui chochote mbele ya mafundi wako na wakatumia mwanya huo kukudanganya baadhi ya vitu.

Anashauri pia kuhakikisha unasimamia ipasavyo ujenzi wa nyumba yako unapoanza hadi unapomalizika ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa badala ya kuwaachia huru mafundi.

# Glasi zinabadili mwonekano wa nyumba

Na Restuta James

WIKI iliyopita nilikukumbusha mambo ya kuzingatia ili uweze kubadili mwonekano wa nyumba au madhari ya nyumbani mwako katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Msomaji wangu aliyejitambulisha kwa jina la Regina Joshua, alinipigia simu na kunipa mbinu nyingi zaidi za namna ya kupamba nyumba hata baada ya sikukuu za mwisho wa mwaka.

Anasema glasi za mvinyo ni pambo zuri katika kubadili mwonekano kwa kutumia kufunika aina fulani za pambo ili kunogesha meza au korido.

Anasema kwa wakati huu wa sikukuu, aina hiyo ya glasi inaweza kutumiwa kufunika vimipira vilivyozoeleka kupamba mti wa Krismasi na kuongeza mvuto.

Regina anasema juu ya glasi iliyofunikwa (kama inavyoonekana pichani), unaweza kuweka mshumaa mkubwa unaotosha kwenye mzunguko huo.

"Mshumaa unatakiwa uenee juu ya glasi. Unaweza kuweka mshumaa mweupe usio na manukato au ukaweka wenye harufu nzuri kadiri utakavyoona inafaa," anasema.

Anasema glasi zinaweza kufunikwa juu ya 'table mats' au kwenye trei nzuri na inapendeza zikiwekwa kwenye meza ya console au kwenye shelfu ya kuwekea picha koridoni.


Anashauri kuwa ukubwa wa glasi ndio utakaoamua aina ya mapambo na kwamba kwenye trei unaweza kuweka mambo lingine kadiri unavyoona inafaa.

"Glasi zisiwe nyingi wala isiwe moja. Nne ni standard kabisa lakini hata tatu zinakaa vizuri. Si lazima ununue mapambo ya gharama kuifanya nyumba yako classic. Glasi ulizonazo ukizitumia vizuri unaokoa gharama na unaonekana wa kisasa," anaongeza Regina.

Tuwasiliane kupitia 0753 333 330 au restutajames@gmail.com



## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
HUU MKONO NIMEVUNJIKA 'GESTI' WAKATI NAREKEBISHA SHOTI YA UMEME 'CHUMBANI' 'NGAZI IKATELEZA!'
KWA HIYO YULE MKE WA MTU NDIO ALIKUWA 'TENESKO' MWENZAKO?
INAONEKANA MKEO HANA WIVU HATA AKIKUKUTA UMEKUMBATIWA KAMA HIVI JAMANI
ANDAA NAULI YANGU UNAKARIBIA KUSHUKA
MWANAUME ETI' UNARINGA KISA MTAANI UNAITWA HENDISAMU!
NA KWELI BABA WEWE UNGEITWA HENDISAMU UNA HAKI YA KUMFUNGA MTU JELA MAISHA!
USINIONE HIVI MIMI NIMEKULA CHUMVI NYINGI YAKUTOSHA!
KWA HIYO UNASUBIRI 'SAFURA?'
KONDA USINISOGELEE UTANIAMBUKIZA MIMACHO YAKO... ONA ILIVYKUWA MIYEKUNDU!
SAWA BASI NAULI ZANGU NITAZIFUATA NIKISHAPONA NASHUKA!
NINI?
UTAIZIFUATA WAPI WAKATI TUMEKUTANA HUMU HUMU? WE MWEHU?
HAYA NIMEWASAMEHE ACHA DEREVA AKAWASHUSHE ATANIKUTA HAPA NAMSUBIRI
KWENDA ZAKO HUKO! SHIKA NAULI YAKO HAPA SIO MOMBASA
KUTOKANA NA MIPANGO YAKO YA KUNIOA INACHUKUA MUDA MREFU...NIMEONA BORA NIOLEWE TU.
AFADHALI OLEWA NIOE!
UMENIPIGA BIA LAKINI SIJALEWA KABISAAA YAANI KAMA NIMEKUNYA MAJI SAFI
KWA HIYO HATA SUMU NILIYOKUWEKEA KWENYE BIA HAITAKUUA?
MVUA ZINAKUJA NA UPEPO HAKULALIKI NDANI NAOGOPA!
MBONA BADO UPO KITANDANI AU UNAJIONA UPO BARAZANI?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...JIEPENDEKEZE UPATE SIFA UKWENI UKATAMBE KWENU

HABARI KIMATAIFA

# Algeria wapiga kura kumchagua rais

**ALGERS,** ALGERIA

WASTANI wa wapiga kura milioni 24 jana walitarajiwa kupiga kura nchini Algeria katika uchaguzi mkuu wa urais.

Rais anayemaliza muda wake, Abdelmadjid Tebboune anawania muhula wa pili na kushindana na wapinzani wake wawili.

Mshindi wa nafasi hiyo atakuwa na jukumu la kutawala nchi hiyo yenye watu milioni 45, na inayoongoza barani HYPERLINK "https://www.rfi.fr/sw/lebo/afrika/" \t "_self" Afrika kwa kuuza nje gesi asilia.

Rais HYPERLINK "https://www.rfi.fr/sw/lebo/abdelmadjid-tebboune/" \t "_self" Abdelmadjid Tebboune kutoka chama cha National Liberation Front (FLN), na vuguvugu la Kiislamu la El Bina, anajipigia upatu kwa kutaka kumaliza mradi wake unaoitwa Algeria mpya.

Hata hivyo, anakabiliwa na wapinzani wawili. Kwa upande mmoja, Abdelaali Hassani, anayewakilisha chama cha Movement of Society for Peace (MSP), na Youssef Aouchiche, kutoka chama cha Front of Socialist Forces (FFS).

**RFI**

# Papa Francis ataka usawa nchini Papua New Guinea

**PORT MORESBY,** POPUA NEW GUINEA

KIONGOZI wa kanisa katoliki duniani, Papa Francis, ameanza ziara yake nchini Papua New Guinea jana kwa kutoa wito wa kutumiwa rasilimali inayopatikana kwenye taifa hilo kwa manufaa ya jamii yote.

Akiwahutubia viongozi wa kisiasa na wafanyabiashara, Papa Francis alisema ni muhimu kwa maliasili zinazopatikana nchini humo ikiwemo madini, vito vya thamani na gesi asilia viwanufaishe watu wote.

Matamshi yake yatachochea mjadala kwenye taifa hilo la Pasifiki ambalo raia wake wengi wanaamini utajiri wao unawanufaisha wachache kwa njia za wizi na ufisadi.

Licha ya utajiri mkubwa wa maliasili, Papua New Guinea ndiyo nchi masikini zaidi kwenye kanda hiyo na kati ya nusu ya raia wake milioni 12 wanaishi kwenye umasikini uliotopea.

**DW**

# Wanaanga wabaki angani, chombo charejea duniani

**WASHINGTON,** MAREKANI

CHOMBO cha anga za juu kinachoitwa Boeing's Starliner kimekamilisha safari yake ya kurudi Duniani, bila ya kuwabeba wanaanga waliokwama angani.

Wanaanga hao Butch Wilmore na Suni Williams kutoka Nasa wamebaki katika Kituo cha Kimataifa cha Anga za Juu kinachoelea anga za mbali baada ya chombo hicho kuwa na hitilafu ya kiufundi.

Boeing Starliner kilijiondoa katika obiti yake na kurejea duniani kikiwa kitupu.

Chombo hicho ambacho kilikumbwa na matatizo ya kiufundi baada ya kurushwa kuelekea angani kikiwa na wanaanga wawili, kilionekana kuwa ni hatari kuwarudisha wanaanga hao duniani.

Badala yake wanaanga hao watarudi kwa kutumia chombo cha SpaceX Crew Dragon, mwezi Februari.

Wakati walipokwenda anga za juu wanaanga hao walitakiwa kukaa kwa siku nane, lakini muda uliongezwa na kuwa miezi minne.

Baada ya Starliner kurejea, msemaji wa Nasa, alisema alifurahishwa na kutua kwa mafanikio kwa chombo hicho, lakini alitamani kama safari hiyo ingeenda vizuri kama ilivyopangwa awali.

Safari ya kurudi ilichukua saa sita, na baada ya kuingia kwenye angahewa ya dunia miamvuli ilitumiwa kupunguza kasi yake ma kutua salama jana usiku katika kituo cha White Sands Space Harborhuko katika jimbo la New Mexico.

**BBC**



Moja ya kambi ya wakimbizi inavyoonekana baada ya kushambuliwa na Israel katika mji wa Gaza jana. **PICHA: REUTERS**

# Wanafunzi 70 watoweka baada moto kuteketeza bweni la shule

**NAIROBI,** KENYA

MAKAMU wa Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua, ametangaza kutoweka kwa wanafunzi 70 baada ya tukio la moto kuunguza bweni la shule ya msingi ya Hillside Endarasha.

Wanafunzi hao hawajulikani walipo mara baada ya moto kuteketeza bweni la shule hiyo iliyoko kaunti ya Nyeri. Akizungumza katika eneo hilo, Makamu wa Rais Gachagua, alisema juhudi za kuwatafuta zinaendelea ili kufahamu mahali waliko.

"Wanafunzi 70 bado hawajulikani walipo, hiyo haimaanishi kuwa wamefariki au wamejeruhiwa. Neno sahihi ni kwamba hawajulikani walipo," alisema Gachagua.

Awali, Rais William Ruto ametangaza siku tatu za maombolezo na kusisitiza ufanyike uchunguzi ili kubaini chanzo cha moto.

Hata hivyo, mwalimu Josaia Mwangi ambaye anafundisha katika shule ya Hillside Endarasha,alisema inakuwa vigumu kuelewa kilichotokea usiku wa mkasa huo wa moto. "Kulikuwa kama hitilafu ya umeme na ghafla moto ulizuka katika bweni la wavulana. Ilikuwa usiku, watoto wengi walikuwa wamelala. Kengele ilisikika, lakini watu wengi hawakuisikia, kwa hivyo uhamishaji wa watoto ulikuwa wa shida sana. Inasikitisha sana, inavunja mioyo yetu, "alisema mwalimu huyo.

Kenya imekubwa na matukio ya moto kuunguza shule kadhaa kuanzia 2001 nadi 2017 na kuua watoto 77.

Silas David Obuhadsa, kiongozi wa chama cha wazazi nchini humo, analaumu kukosekana kwa ubora kwa shule zenye mabweni.

"Baadhi ya shule zina mabweni yanayofanana na magereza, madirisha yamefungwa, milango imefungwa kwa nje. Kwa hiyo moto ukizuka katika bweni la aina hii, hakuna njia za kutoka ambazo watoto wanaweza kupitia na athari zake ni kubwa sana, kuanzia na vifo vya wanafunzi. " alisema

**DW**

MAKALA

# MAWAZO HAYAPIGWI RUNGU



Na Magabilo Masambu

**Bahati mbaya katika maisha yetu ya kila siku, tunahangaika sana na mabaya kuliko mema. Wako watu wanaoshauri mambo mema sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi lakini, kwanza hawajulikani na hakuna siku wamepata hata simu kutoka kwa viongozi serikalini...**

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Mrisho Kikwete, katika hafla ya kumbukumbu ya miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, akieleza kisa cha mgomo wa wanafunzi wa chuo kikuu mwaka 1978 kupinga wabunge kujiongezea mshahara, akimnukuu Nyerere alisema: "Mawazo hayapigwi rungu, badala yake mawazo hushindwa na mawazo yaliyo bora zaidi."

Haya ni maneno aliyoyasema Mwalimu Nyerere baada ya mtazamo wa viongozi wengi kuona kama mgomo ule wa wanafunzi ulikuwa uhaini wakipendekeza wanafunzi wale watiwe kizuizini.

Hapo ndipo Mwalimu alipowapinga na kuwaeleza kwamba hoja hujibiwa kwa hoja bora zaidi na si kutumia rungu au nguvu.

Leo nimeona tujikumbushe haya. Nguvu katika kujibu hoja ni kama zinataka kutawala zaidi kuliko kutumia hoja kujibu hoja.

Ni jambo hatari sana tunaposhindwa kujibu hoja za watu kwa hoja badala yake zinatumika njia zingine ambazo zinaweza kuhatarisha amani ya nchi huko tunakoelekea. Kwa sababu tunaipenda nchi yetu iendelee kuwa na amani na utulivu, tunao wajibu wa kuyasema haya.

Viongozi tukishazoea kutumia nguvu kujibu hoja, uwezo wa viongozi wengi katika kujenga hoja unafifia. Wanakuwa kama wanafunzi ambao wanasoma huku wakiwa na matumaini ya kuonyeshwa mitihani kwa maana hawatajifunza kwa bidii. Sifa kubwa aliyokuwa nayo Mwalimu Nyerere, inatajwa kuwa ilikuwa uwezo mkubwa na thabiti wa kusikiliza hoja na kuzijibu kwa ustadi mkubwa. Jambo hili haliji tu kwamba umezaliwa nalo, bali ni mazoea ya kukabiliana na hoja za mara kwa mara na mwishowe zinakujenga kuwa mahiri.

Katika Makala zilizotangulia, nimewahi kushauri kwamba njia bora kabisa ya kupunguza au kumaliza kile kinachoitwa ukosoaji bila madhara yoyote ni kupuuza mengi yasiyo ya kweli ama kuyajibu kwa hoja.

Ukosoaji ni dhana inayotengenezwa na anayedhani kwamba anakosolewa, wakati upande wa pili kwa anayechukuliwa kama mkosoaji huona kama anachokisema ni ushauri ili jambo fulani likae kama anavyotaka liwe.

Kwa hiyo tafsiri ya kile kinachosemwa kinaweza kuitwa ama ukosoaji au ushauri kutegemeana na anayekipokea.

Anayeambiwa siku zote ndiye mwenye uchaguzi wa kukipa jina ama achukulie kama ukosoaji au ushauri kwake ambao pia anaweza kuufanyia kazi au kuuachana nao, kutokana na mazingira ya jambo analosemwa nalo.

Bahati mbaya katika maisha yetu ya kila siku, tunahangaika sana na mabaya kuliko mema.

Wako watu wanaoshauri mambo mema sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi lakini, kwanza hawajulikani na hakuna siku wamepata hata simu kutoka kwa viongozi serikalini ya kupongezwa kwamba wanafanya kazi nzuri. Siku wakiamua kutukana ndiyo siku watakayojulikana kwamba kumbe wapo.

Labda niwashirikishe kisa hiki. Tukiwa sekondari tulikuwa na mwalimu wetu wa somo la Kiswahili, ambaye pia alikuwa refa wa mpira wa miguu.

Siku moja alipigwa uwanjani na akakimbia, asubuhi yake alipokuja darasani, mwanafunzi mmoja akatunga sentensi kwamba "refa alikimbizwa uwanjani" mwalimu huyo akajibu, je refa alikamatwa au hakukamatwa? Darasa zima tukaitikia kwa vicheko na vifijo kwamba hakukamatwaaa! Jambo hilo likawa limeishia hapo, tukacheka tukafurahi na mwalimu pia akacheka maisha yakaendelea.

Kwa hiyo kuna namna nyingi za kuyamaliza mambo, si kila jambo ni lazima kulimaliza kwa kutumia nguvu.

Jambo fulani likizungumzwa likapuuzwa huwa mzungumzaji haendelei tena.

Lakini yale tunayoona kwamba ni kweli hatufanyi vyema na yanahitaji mabadiliko kwa maslahi ya nchi ni kuyafanyia kazi, bila kujali kwamba anayeyasema ni nani.

Mara zote tukipenda kusikia mazuri tu kutoka kwa marafiki zetu wa karibu hatutapata kujua madhaifu yetu.

Badala yake tutapata habari za kufurahisha pekee ili tuwape vyeo wanaotufurahisha na ni vigumu sana kuendelea kimawazo kwa sababu tunakuwa tumejifungia.

Ndani ya ukosoaji kuna ushauri na anayekushauri anaweza kukushauri vibaya au vizuri, hivyo uchaguzi ni wako kutumia ushauri utakaoleta manufaa kwako na kuacha ule unaodhani ni mbaya.

Kutumia nguvu katika kujibu hoja kunazuia hata mawazo mazuri yenye kuleta maendeleo kwa sababu kila mtu anakuwa na hofu kwamba inawezekana akishauri hivi yule au huyu hatapenda.

Mwisho wa siku watakuwa wanaona mambo yanaharibika na wanaacha ili uharibikiwe Zaidi. Wale wanaokusifu kila mara, lazima ujiridhishe kama sifa wanazokupa unastahili au kuna mambo wanayataka kutoka kwako kwa kukusifu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mayasa kaharibiwa na mkorogo, akamkasirikia Marijani Rajabu*



Na Adam Fungamwango

**Kuna wanawake ambao kwa sasa tunaona wanajichuna ngozi na kutumia dawa ili kuondoa rangi yao halisi nyeusi na kutaka waonekane weupe, ikienda sambamba na kuweka nywele bandia ili zionekane ndefu, na kuzificha zile halisi za kipilipili. Yoe hayo yalikuwapo enzi hizo.**

HAKUNA ambacho hakijafanyika chini ya jua. Kila kinachofanyika sasa kimeshawahi kufanywa miaka mingi iliyopita.

Kama unawaona watu wabaya na makatili sasa, basi huko nyuma wameshawahi kutokea zaidi ya hao unaowaona, wakiongozwa na Adolf Hitler, aliyekuwa kiongozi wa Ujerumani wakati huo.

Kama unaona wanawake warembo leo, basi maelfu ya miaka iliyopita kulikuwapo na msichana mmoja anayesadikiwa kuwa ndiye mrembo kuliko wote duniani mpaka sasa na haijatokea tena.

Huyu si mwingine bali ni Cleopatra aliyekuwa mtawala wa Misri, miaka 51 mpaka 30 kabla ya kuzaliwa Yesu Kristo.

Hii ni mifano michache tu ya kuonesha kuwa hakuna chochote kiwe kizuri au kibaya kinachotokea leo, halafu kikawa kipya. Hata watu kujibadili rangi kwa kutumia vipodozi walifanya miaka hiyo licha ya kwamba siku hizi wanaita mkorogo.

Siku hizi tunawaona kinadada warembo, wakiwa wamejipamba na kujiremba kiasi cha kuwatetemesha wanaume, lakini huko nyumba unaambiwa wasichana wa zamani akiwemo hata huyo Cleopatra, walikuwa wakijipamba kwa mikufu ya almasi na dhahabu, yakuti na marijani.

Yaani hawa miili yao ilijaa madini halisi matupu, tofauti na hawa wa sasa wa kwenda saluni na kuvaa bangili feki.

Kuna wanawake ambao kwa sasa tunaona wanajichuna ngozi na kutumia dawa ili kuondoa rangi yao halisi nyeusi na kutaka waonekane weupe, ikienda sambamba na kuweka nywele bandia ili zionekane ndefu, na kuzificha zile halisi za kipilipili. Yoe hayo yalikuwapo enzi hizo.

Tabia hii imewaletea shida baadhi yao kwa kuharibika ngozi na hata uzuri wao wa asili pia wanaupoteza. Wengine sasa wanajuta kwa kile walichokifanya wakati wakiwa wasichana. Waswahili wanasema ujana maji ya moto.

Baadhi wanadhani kuwa tabia hii ni ya wasichana na wanawake wa kizazi cha sasa.

Si kweli. Tabia hii ya kujichubua kwa kinadada, kama nilivyosema ilianza mapema miaka ya 1970, labda tu hawakuwa wengi kama ilivyo hivi sasa.

Kipindi hicho wanaojichumbua ni wale kwenye pesa zao tu na wanahesabika.

Kwa sababu gharama yake ilikuwa kubwa sana kutokana na vipodozi kuingia nchini kwa magendo, si kama sasa kila duka lina losheni, sabuni, krimu, manukato na mengine yanayofanana na hayo.

Vipodozi hivyo vilikuwa vikiangizwa kutoka Burundi, Uganda na Kenya.

Na huko kote vilikuwa vikitoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, enzi hizo ikiitwa Zaire.

Wanawake waliovipata ni wale wa matawi ya juu tu na ilionekana sana kwa wanaliokuwa wanaishi Ilala, Magomeni na Kariakoo, yaani kinadada wa mjini tu na si kila mtu kama ilivyo sasa.

Ndiyo maana mwanamuziki Marijani Rajab miaka hiyo ya mwanzoni mwa 1980, alitunga wimbo aliouita, 'Uzuri wa Asili' na mashabiki wanaupa jina la Mayasa.

Marijani ambaye alikuwa akiishi mtaa wa Somali, alishuhudia dada mmoja aitwaye Mayasa, ambaye alikuwa amekoboka sura kutokana na matumizi makubwa ya vipodozi.

Kutokana na tukio hilo, akatunga wimbo huo. Yeye akajionesha ni shoga wa mwanadada huyo aliyepatwa na janga hilo.

Hebu pitia mashairi haya ndiyo ujue hata miaka ya 1980, mikorogo ilikuwapo lakini haikuwa kwa kila mwanamke, zaidi ya wale wadada wa mjini na wajanja tu.

"Mayasa mbona wanichana mabavu bibi ee, sura yako mbona sasa imekuwa hivyo? Nakuuliza mbona hata kunijibu hutaki? Umenisaksirikia kama mimi ndiyo nilikutuma. Sura yako na ulivyokasirika mama ee, ndiyo mimi wazidi kunichana mbavu Mayasa ooo."

"Dada yako jana alipita kunieleza, lakini mimi hata kidogo sikumuamini. Kaniambia ulizidisha tamaa ya urembo, mawazo yako uwe mzuri kuliko ulivyoubwa. Mayasa tizama ulivyobadilika, urembo umekubaldisha sura yako hooo.

"Nasikia ukachanganya madawa ya nywele, ukaona bado na mengine madawa ya ngozi, mchana kutwa hubanduki kwenye kioo, sujui mama ulitaka uwe sawa malaika, Mayasa tuzama nywele zilivyoharibika, sura yako hapo zamani haikuwa hivyo hooo."

*"Oooh Mayasa, mama Mayasa, oooh Mayasa, uzuri ni wa kuzaliwa nao.*
*Oooh Mayasa, mama Mayasa aaa, hapo zamani mama, ulikuwa mwenye umbo la kupendeza.*
*Oooh Mayasa, dada Mayasa aaa, aliyekuona zamani, akikuona sasa atashangaa.*
*Oooh Mayasa, mama Mayasa aaa, tazama sasa dada, uzuri wako wa asili waupoteza.*
*Oooh Mayasa, mama Mayasa aaa, nakwambia kweli mama, aliyekuumba si mjinga."*

Wimbo huu unaonyesha kuwa mikorogo ilikuwepo tangu enzi hizo, pia alishatahadharisha madhara yake kwa vizazi vyote.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Aka Simtaki-10

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda. Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka. Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

SHUKURU alisikia kuwa mpenzi wake amerejea na kumbe hakutoroshwa na Fotu, bali alitoroka mwenyewe kwa kulazimishwa kuolewa.

Hili lilimpa nguvu kutaka kwenda nyumbani kwao. Aliona kama alitoroka na sasa amepatikana inawezekana wazazi wake hasa baba yake akaamua kusalimua amri. Hakuwa hivyo. Akaishia kutimuliwa na mzee Chilambo.

Kurejea kwa Shani kulimfanya mzee Chilambo na ndugu zake kuendelea na matayarisho ya harusi. Upande wa mwana harusi ukapelekewa taarifa kuwa ujiandae. Ni baada ya mahari kubwa kulipwa. Ilivunja rekodi ya vijiji vyote vya Ugalla. Kama utamaduni ya harusi nyingi kwa sasa, hasa za watu wanaojiweza. Mialiko ikaanza na kadi zikaanza kutembezwa katika kijiji cha Mtapenda ambacho anatoka bwana harusi na kile cha Lalangulu cha bi harusi. Pia vijiji jirani navyo ndugu na marafiki walialikwa kwenye harusi hiyo, kikiwemo cha Ilembo ambacho anatoka Salum na dada yake Dora.

Taarifa hizo pia zikamfikia Shukuru. Ilikuwa ni taarifa mbaya kuwahi kutokea maishani mwake. Kuambua tarehe na siku ambayo mpenzi wake aliyetarajia kumuoa yeye anaolewa na mwanaume mwingine.

Hakuamini anachokisikia. Kila kitu kwake aliona kama ndoto. Yote aliyofanyika aliona kama yanaweza kufeli kwa sababu aliami Shani anampenda kwa dhati na asingeweza kamwe kuolewa na mwingine hata kama baba yake atalazimisha. Binafsi aliona maisha yake yaliyobaki bila ya kuwa na Shani hayatokuwa na thamani tena.

Afadhali kama angekuwa amefariki angeweza kushukuru Mungu, lakini kwa mtu anayempenda, yupo hai, akimuona yupo na mtu mwingine, akimpikia, kumfulia, kumtunza na kumfanyia kila kitu kama mumewe yeye akishuhudia, hakutaka kukutana na kitu kama hicho. Akawa anawaza ni kitu gani anaweza kufanya ili kuepuka kushuhudia kitu kama hicho. "Niondoke hapa kijiji?" Akawaza.

*******************************

"Jamani jamani Shukuru kajinyonga..." Ilikuwa ni sauti kubwa kutoka kwa kijana aliyekuwa anakimbia akipita nyumbani kwa mzee Chilambo. Mzee huyo alikuwa nje alikuwa anasafisha mabuti yake ya mvua na kulimia yalikuwa na matope.




**"Amekufa?" Baadhi ya watu wakauliza. "Mimi ndiyo wa kwanza kumuona akiwa anajinyonga, alipojitundika tu na kuanza kuning'inia, nilipanda haraka juu ya kukata kabla aliyojinyongea akaanguka chini, sasa sielewi kama atakuwa amefariki au la." Kijana mmoja akatoa ushuhuda.**

"Nini we mtoto?" Akauliza mzee Mzee Chilambo na kusababisha kijana yule aliyekuwa akikimbia kwa woga bila mpangilio wowote kusimama. "Nimetoka kule." Akaonyesha kidole. "Watu wameshaanza kujaa Shukuru kajinyonga. "We muongo!" "Ndiyo kwenye we nenda baba Shani watu waanza kujaa.' Alisema mtoto huyo kwa sauti kubwa na kuanza kukimbia tena kuelekea nyumbani kwao. "Nani kajinyonga?" Ilikuwa ni sauti iliyotoka ndani kwake. Ilikuwa ya mkewe. "Wapumbavu nyinyi, nione mtu atoke hapa, mtanitambua." Akawapiga mkwara mkewe na binti yake waliokuwa ndani. "Jamani nimesikia kama Shukuru kajinyonga." Bi. Hanifa akaongea kwa sauti ya woga. "Ndiyo mtu wenu huko kajinyonga. Mbona hata siamini, naenda kuthibitisha huko huko." Akasema mzee Chilambo. Lakini akaona haitoshi, akaamua kuwafungia kwa nje ili asitoke mtu. Akaanza kuelekea kule alikoonyeshwa kuwa kuna tukio. Alipofika alikuta tayari watu wameshamtoa alipokuwa ananing'inia juu ya mti na kumuweka kwenye mkeka. Kila mtu akawa anamuangalia yeye. Kila mmoja hapo alijua sababu ya Shukuru kujinyonga. Hakujali aliungana na wale waliokuwa wanatazama tukio.

"Amekufa?" Baadhi ya watu wakauliza. "Mimi ndiyo wa kwanza kumuona akiwa anajinyonga, alipojitundika tu na kuanza kuning'inia, nilipanda haraka juu ya kukata kabla aliyojinyongea akaanguka chini, sasa sielewi kama atakuwa amefariki au la." Kijana mmoja akatoa ushuhuda. "Nasikia, kujua kama amefariki au la ni lazima apelekwe kwenye zahanati ya kijiji ili madokta wakathibitishe." Alisema mzee mmoja na wote wakakubaliana na hilo. Mwanakijiji mmoja alikuwa na bodaboda ya miguu mitatu. Ni ile ambayo mbele ni bodaboda, lakini nyuma imeinganishwa kama toroli. Shukuru akalazwa nyuma na wazee wengine wawili, pamoja na baba yake tayari kwenda kumfanyia uchunguzi kama yupo hai au la.

Hata hivyo, vifaa ya zahanati hivyo vilikuwa duni kiasi cha kushindwa kuthibitisha kama mgonjwa alikuwa hai au amefariki dunia, hivyo moja kwa moja ikaamriwa apelekwe haraka hospitali ya Mpanda mjini.

*******************************

Tukio lile hakumfanya mzee Chilambo kuahirisha mpango au maandalizi ya harusi kati ya binti yake Shani na kijana Fotu kutoka kijiji cha Mtapenda.

Ilipangwa kufanywa siku tatu baadaye baada ya tukio la Shukuru kujinyonga. Wakati wazazi, ndugu na baadhi ya majirani ya karibu wanashukulikia vipimo kujua kama Shukuru yupo hai au la mjini Mpanda, mzee Chilambo na ndugu zake waliendelea na taratibu za kuozesha. Moyoni mzee huyo alifurahi ingawa hakutaka furaha yake kuionyesha bayana. Alijua kabisa kuwa sasa binti yake ataolewa kwa moyo mmoja na kijana wa kitajiri Fotu kwani yile masikini haijulikani kama amekufa au yupi hai. Hiyo kwake haikumsumbua. Watu walikusanyika siku ya sherehe. Ndugu na bi harusi na bwana harusi walifika nyumbani kwa mzee Chilambo kwa ajili ya kufunga ndoa.

Sherehe kabambe ya kifahari ilitarajiwa kufanyika kijiji cha Mtapenda kwenye ukumbi mmoja uliopangwa.

Kila kitu kilikwenda kama nilivyopangwa. Kabla ndoa haijafungwa, ikaja habari kuwa Shukuru yupo hai.

Ililetwa na mbea mmoja, shoga yake Shani ambaye kutokana na urafiki wao alifanikiwa kujipenyeza mpaka chumbani. Akamwambia taarifa za uhakika alizozipata kutoka Mpanda, ni kwamba Shukuru yupo hai, kumbe hakufa kwenye lile jaribio la kutaka kujitoa uhai. Vipimo vya hospitali ya Mpanda vilionyesha kuwa alikuwa amezirai tu kutokana na kukosa hewa kwa muda fulani, pamoja na kuanguka kutoka juu ya mtu, baada ya kijana mmoja mwanakijiji cha Lalanguru kufanya kazi hiyo ya kumuokoa.

"Hivi huna habari?" Mbea huyo alimnong'oneza sikioni ili wengine wasisikie. "Habari gani tena?" "Za Shukuru?!!" Kusikia jina hilo, Shani alishtuka. Hakusema kitu akabaki anamtazama shoga yake. "Kumbe yupo hai, hajafa, nimepata taarifa na hivi sasa anapatiwa matibabu ya majeraha tu ya kuanguka, ni mzima dada."

"Ni mzima?" Shani akauliza mwenyewe. Akajiuliza jinsi Shukuru atakapojisikia kama akirejea na kukuta tayari ameshafunga ndoa ya Fotu. Yeye mwenyewe hakuna tayari na ndoa ile ni kwa sababu tu ya baba yake.

Akajiona msaliti. Mtu ambaye aliamua ajitoe uhai kwa ajili yake. Kwa sababu ya kumpenda. Ni upendo gani aliokuwa nayo kwake Shukuru. Binafsi alimpenda sana Shukuru, na anajua Shukuru anampenda sana, ila mazingira ndiyo yamekataa.

Wakati huo huo, alikuja mama mmoja akamwinua kwa ajili ya kumpeleka akashikane mikono na mpenzi wake kabla ndoa haijafungwa. Mawazo yalikuwa mengi kichwani. Hakujua afanye nini. Akanyanyuka kwa tabu. Akatembea kwa kujikongoja. Akapelekwa kwenye chumba ambayo aliwepo Fotu. Ndiyo mara ya kwanza alikuwa anamuona. Alikuwa kijana wa kitajiri aliyependeza kwa suti kali na viatu nyeusi vilivyong'aa kwa dawa. Hiyo haikumshawishi Shani. Kijana alisimama kwenda kumlaki mke mtarajiwa. Kabla hata hajafanya hivyo, Shani alianguka chini pepe yake bila kuguswa na mtu.

Itaendelea Jumapili

# STEVO UTAMUWEZA KAJALA?

MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Stephen Odera, maarufu kama Stevo Simple Boy, amemkaribisha mrembo kotoka Tanzania Kajala Masanja kwenda kupamba nyumba yake ikiwamo kumpikia chakula kizuri.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, alichapisha video iliyomuonesha akipika chakula aina ya samaki na kuelezea hamu yake ya kuona siku moja Kajala anachukua nafasi ya kukaa jikoni.

"Kajala, Kajala Kajala, mazee mi nimedata kwako, na tena umenivutia. Kajala tafadhali njoo unipikie, unioshee vyombo, unipangie nyumba," alisema.

Stevo Simple Boy anaishi peke yake baada ya kutengana na aliyekuwa mke wake, Grace Atieno.





## HAKUNA KAMA NANDY

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Nandy amezidi kuonesha umwamba wake baada ya kuendelea kuweka historia ya kuwa msanii wa kwanza wa kike kuandaa tamasha kubwa la muziki nchini.

Jana mkoa wa Kigoma, ulitingishwa na burudani ya aina yake baada ya wasanii kibao wa muziki kupanda jukwaani katika Nandy Festival 2024 ambapo kwa mwaka huu mkoa huo ulifungua dimba.

Katika historia ya muziki Nandy ndiye mwanamuziki wa kike aliyeweza kumudu kuandaa tamasha kubwa la kimataifa la muziki katika mikoa mbalimbali akiwa na orodha ya mastaa kibao.

## ZISIKUPITE

### NEWCASTLE NA ALANGA JANUARI

KLABU ya Newcastle inaweza kutazama upya mpango wa kumnunua fowadi wa Nottingham Forest na Sweden, Anthony Elanga mwenye umri wa miaka 22, Januari. (**Football Insider**)

### DEPAY ATUA CORINTHIANS

KLABU ya Corinthians inakaribia kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 30, ambaye ni mchezaji huru. (**Globo**)

### VAN DIJK KUONGEZEWA MUDA

LIVERPOOL ina nia ya kumpa mkataba mpya mlinzi wa Uholanzi, Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 33, ili kuongeza muda wake wa kucheza Anfield zaidi. (**Football Insider**)

### MANGAN KUMFUATA ANCELOTTI

KOCHA msaidizi wa Stockport County, Andy Mangan anatazamiwa kuwa msaidizi wa Carlo Ancelotti katika klabu ya Real Madrid. (**Athletic**)

### BARCA KUKOMAA NA WILLIAMS

BARCELONA inatazamiwa kufufua azma yao ya kumnunua mshambuliaji wa Athletic Bilbao, Nico Williams mwenye umri wa miaka 22, raia wa Hispania. (**Sport**)

### MEDINA KUTUA FENERBAHCE

KLABU ya Fenerbahce inayonolewa na Jose Mourinho imekubali kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Cristian Medina mwenye umri wa miaka 22 kutoka Boca Juniors ifikapo mwezi Januari. (**Fabrizio Romano**)

### CASEMIRO, ERIKSEN KUTOLEWA

MANCHESTER United inataka kuwatoa kwa mkopo kiungo Casemiro mwenye umri wa miaka 32 na Christian Eriksen, ambao wanachezea Brazil na Denmark. (**Givemesport**)

### ONUACHU AMEKATAA

MSHAMBULIAJI wa Nigeria na Southampton, Paul Onuachu mwenye umri wa miaka 30, amekataa kuhamia Goztepe ya Uturuki. (**Sabah**)

### KOVACIC HAJUI HATIMA YAKE

KIUNGO wa kati wa Croatia, Mateo Kovacic mwenye umri wa miaka 30, anafikiria mustakabali wake Manchester City kufuatia kurejea kwa Mjerumani, Ilkay Gundogan mwenye umri wa miaka 33, katika nafasi hiyo hiyo. (**Football Insider**)

### CABAL AWANIWA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United inamfuatilia kwa karibu beki wa kushoto wa Juventus mwenye umri wa miaka 23 kutoka Colombia, Juan Cabal. (**Tutto Juve**)

### ERIKSEN ALITAKIWA REAL BETIS

KLABU ya Real Betis ilitoa ofa kwa kiungo wa kati wa Manchester United na Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 32, siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho. (**Fabrizio Romano**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MEMPHIS DEPAY ATUA CORINTHIANS YA BRAZIL

**SAO PAULO,** Brazil

**Nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi anajiunga na klabu hiyo kwa mkataba wa miaka....**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Uholanzi, Memphis Depay amekamilisha mkataba kujiunga na Klabu ya Corinthians ya Brazil kwa uhamisho huru, kwa mujibu wa ESPN.

**Depay mwenye umri wa miaka 30, anajiunga na klabu hiyo yenye maskani yake Sao Paulo kwa mkataba wa miaka miwili.**

Anatarajiwa kuwasili Brazil wiki ijayo na kutambulishwa rasmi kwa mashabiki wa timu hiyo kabla ya mechi ya Copa Brasil dhidi ya Juventude siku ya Alhamisi.

Baada ya kufunga mabao 13 katika mechi 22 alizoanza Barcelona msimu wa 2021-23, alijiunga na Atlético Madrid msimu uliopita na alifanikiwa kufunga mabao tisa katika mechi 12 alizoanza.

Msimu wake bora wa klabu ulikuja 2014-15 akiwa na PSV Eindhoven, ambapo alikuwa mfungaji bora akiwa na mabao 22 na asisti tano.

Kiwango hicho kiliivutia klabu ya Manchester United na kumsajili kwa uhamisho wa Euro milioni 34, lakini muda wake Old Trafford ulijaa matatizo ndani na nje ya uwanja.

Alifunga mabao saba pekee na asisti tatu katika mechi 45.

Depay amekuwa mchezaji muhimu wa timu ya taifa ya Uholanzi, akifunga mabao 46 katika mechi 98 tangu 2013.

Ndiye mfungaji wa pili wa muda wote wa nchi hiyo nyuma ya Robin van Persie.

## HABARI MICHEZO

# KANE: SASA NALITAKA KOMBE LA DUNIA 2026

**LONDON,** England

HARRY Kane amekiri kuwa bado hajaweza kupona kikamilifu maumivu ya kichapo cha England katika fainali ya Euro 2024 dhidi ya Hispania lakini akaapa kutumia hali hiyo kama "moto ndani ya tumbo langu" kushinda Kombe la Dunia la 2026.

Simba Watatu hao walipokea kichapo cha pili mfululizo katika fainali ya Euro mapema msimu huu wa majira ya joto wakati Nico Williams na mchezaji wa akiba Mikel Oyarzabal walipoipatia Hispania ushindi wa 2-1 mjini Berlin nchini Ujerumani.

Kocha Gareth Southgate alijiuzulu muda mfupi baadaye na England kuanza enzi mpya chini ya kocha wa muda Lee Carsley kwa pambano la Ligi ya mataifa ya Uefa dhidi ya Jamhuri ya Ireland huko Dublin jana Jumamosi.

Na Kane alisema: "Nadhani tulifanya vizuri sana kufika fainali. Nadhani hayakuwa mashindano rahisi. Sidhani tulifika viwango katika michezo mingi ambayo tunajua tunaweza.

"Lakini jambo chanya kutoka kwa hilo ni kwamba tumefika fainali. Kila inapoisha hivyo, kwa kushindwa, kila mtu anaondoka haraka na inarudi kwenye maisha yako mwenyewe. Unajaribu kupata mapumziko lakini kabla ya kujua, unarudi. kwa msimu mpya.

"Huwezi kuimaliza kabisa lakini nadhani unaendelea na unaangalia maeneo ambayo unaweza kuboresha kutoka kwa mtazamo wa kibinafsi na unajaribu kutekeleza hilo katika msimu mpya.

"Kama timu, tunaweza kuchukua mambo mengi mazuri kutoka kwa majira ya joto, mazuri mengi kutoka kwa miaka minne iliyopita. Lakini mwishowe ni kuboresha na kuna maeneo ambayo tunaweza kuboresha, haswa katika michezo tunapoangalia nyuma.

"Hiyo sasa ni kazi yetu kama wachezaji, kujaribu na kuwa bora zaidi. Michezo hii na kambi chache zinazofuata ni fursa nzuri ya kufanya hivyo.

"Kila kushindwa ni tofauti kwa njia yake. Ni ngumu. Unapokaribia kufikia moja ya kilele cha taaluma yako ya kimataifa na ikachukuliwa kama hivyo, ni ngumu sana. Lakini mwishowe, maisha yanasonga mbele.

"Kwa mtazamo wangu, inanipa motisha zaidi, inaweka moto tumboni mwangu kujaribu kurejea huko tena au Kombe la Dunia na kuwa na matokeo tofauti wakati huu."

Carsley alianza jukumu lake jipya kwa kukabiliana na nchi ambayo aliichezea mara 40 kama mchezaji, moja tu ya viungo vingi kati ya pande hizo huku Jack Grealish na Declan Rice wakibadilisha utiifu kutoka Ireland hadi gereza mapema katika maisha yao ya soka.

Alipoulizwa kama alikuwa na wasiwasi kuhusu kuanzisha wawili hao kwenye Uwanja wa Aviva, Carsley alisema: "Hapana, hata kidogo. Hatukuzungumza na Jack na Declan pekee bali na kikosi kizima."



## Bruyne alia na FIFA, UEFA

**BRUSSELS,** Ubelgiji

KIUNGO wa kati wa Manchester City na nahodha wa Ubelgiji, Kevin De Bruyne alisema fedha huzungumza zaidi na FIFA na UEFA huku akiibua wasiwasi juu ya athari za kalenda iliyojaa kwenye afya na uchezaji wa wachezaji.

Mashindano yote matatu ya Klabu ya Ulaya yamepanuliwa hadi timu 36 msimu huu na vyama vya wanachama vya FIFPRO vya Ulaya vimeanza hatua za kisheria dhidi ya FIFA kuhusu kupanuliwa kwa Klabu bingwa ya Dunia kwa timu 32, kuanzia Juni ijayo nchini Marekani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 aliulizwa ikiwa ana wasiwasi kuhusu kuongezwa kwa mechi kwa Klabu na mashindano ya kimataifa.

"Tatizo la kweli litaibuka baada ya Kombe la Klabu bingwa ya Dunia," alisema De Bruyne akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi ya Ijumaa ya Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Israel.

Ubelgiji ilishinda kwa mabao 3-1 huku De Bruyne akifunga mara mbili.

"Tunajua kutakuwa wiki tatu pekee kati ya fainali ya Kombe la Klabu bingwa ya Dunia na mechi ya kwanza ya Ligi Kuu. Kwa hivyo, tuna wiki tatu za kupumzika na kujiandaa kwa mechi nyingine 80."

Mnamo Julai, chama cha wachezaji wa kulipwa FIFPRO kilisema kinawasilisha malalamishi kwa wadhibiti wa kutoaminika wa Umoja wa Ulaya kuhusu kalenda ya mechi za kimataifa za FIFA.

Ripoti iliyotolewa na FIFPRO siku ya Alhamisi ilisema baadhi ya wachezaji wana angalau asilimia 12 ya mwaka kupumzika, ambayo ni matokeo ya waandaaji wa mashindano kutoweka kipaumbele kwa ustawi wa wachezaji.

"Labda mwaka huu mambo yatakuwa sawa, lakini mwaka ujao kunaweza kuwa na matatizo. Chama cha Wanasoka wa Kulipwa nchini Uingereza na vyama vingine vya wachezaji vimejaribu kutafuta suluhu," aliongeza.

"Suala ni kwamba UEFA na FIFA wanaendelea kuongeza mechi za ziada, na tunaweza kuibua wasiwasi, lakini hakuna suluhu iliyopatikana. Inaonekana kwamba fedha huzungumza zaidi kuliko sauti za wachezaji."

## Deschamps: Uzoefu ulitumaliza kwa Italia

**PARIS,** Ufaransa


KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps alizungumza kabla ya mchezo wa Ijumaa na Italia kuhusu kuwajaribu wachezaji wapya kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa ya Uefa, na baada ya kufungwa 3-1 huko Paris, mpango huo haujabadilika.

Deschamps alikosolewa vikali baada ya Euro 2024, ambapo, licha ya timu yake kufika nusu fainali, walishindwa kutamba, na dhidi ya Italia alimpa fowadi Michael Olise mechi yake ya kwanza, na pia alimleta kiungo Manu Kone kwa mechi yake ya kwanza.

"Ni suala la usawa, timu ni changa na wengine wameanza mechi zao za kwanza leo (juzi)," alisema Deschamps.

"Ninajua kwamba kwa kutoweka timu inayoanza uwanjani nilijihatarisha na hii iliharibu utendaji kwa jumla."

Katika michuano ya Euro, Ufaransa iliruhusu mabao matatu katika mechi sita walizocheza, lakini ikaruhusu mabao matatu nyumbani dhidi ya Italia ambapo Deschamps aliwaacha Jules Kounde na Dayot Upamecano kwenye



benchi huku Ibrahima Konate na Jonathan Clauss wakianza badala yao.

"Ulinzi umebadilika, nilishasema hivyo. Wakati umefika wa kuwapa nafasi ya kucheza wachezaji wengi iwezekanavyo na usiku wa leo mbele ya wapinzani wa kiwango cha juu," alisema.

"Katika mchezo ujao maono hayo ya mambo hayatabadilika, ni wakati wa kufanya hivyo."

Ufaransa walianza vyema, huku Bradley Barcola akiwaweka mbele baada ya sekunde 12, lakini wakaruhusu Italia kurejea mchezoni na kushindwa kukabiliana na mbinu za wapinzani.

"Tulikuwa na mwanzo mzuri baada ya bao, mara moja tukaweka shinikizo kwa mpinzani, lakini mambo yakawa magumu zaidi," aliongeza Deschamps.

"Kuna mabao pia kuna makosa, lakini usiku wa leo (juzi) kwa mtazamo wa mchezo tulikuwa tumekosekana katika sehemu ya pili ya kipindi cha kwanza.

"Kipindi cha pili tulianza tena kwa nia nzuri, lakini baadaye wakafunga bao lingined kwa kiwango hiki cha chini Italia waliweza kucheza kwenye kaunta."

Deschamps ana muda mchache wa kuweka mambo sawa na wanahitaji kumaliza hasara hii haraka huku Ufaransa wakiwakaribisha Ubelgiji Jumatatu.

"Kushindwa huku kunaumiza kila mtu usiku wa leo (juzi). Siku zote naangalia ukweli, bila kujali mazingira," alisema Deschamps.

"Hongera kwa Italia, walifanya kile ambacho kilitakiwa kufanywa ili kushinda. Tulikuwa na mapungufu na sasa tunapaswa kujiandaa kwa Ubelgiji."

## HABARI MICHEZO

# MOROCO: TUNAKWENDA KUSHAMBULIA UGENINI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa timu ya soka ya taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars', Hemed Suleman 'Moroco', amesema katika mchezo utakaochezwa Jumanne dhidi ya timu ya taifa ya Guinea, watashambulia zaidi tofauti na ilivyokuwa mchezo wa kwanza dhidi ya Ethiopia wa kufuz fainali za AFCON 2025.

Akizungumza muda mfupi kabla ya kukwea pipa kuelekea nchini Ivory Coast ambako itachezwa mechi hiyo ya pili ya kusaka tiketi ya kucheza fainali hizo, Moroco alisema wamefanyia kazi mapungufu yote yaliyojitokea kwenye mchezo uliopita.

"Huko tunakokwenda tunakwenda kushambulia, huo ndiyo mfumo tutakaotumia, kwa sababu hakuna kingine tena, tunahitaji pointi tatu.

> **Siamini sana nyumbani au ugenini, mpira siku hizi unachezwa popote pale, kwa jinsi tulivyocheza mechi iliyopita kipindi cha pili na tumerekebisha na makosa tuliyoyaona, tuna uhakika wa kushinda,"alisema Morocco.**

Alisema pamoja kwamba anakwenda kushambulia zaidi kuliko kuzuia, lakini anaamini kuwa mchezo huo utakuwa mgumu kwani Guinea ni timu ngumu ambayo walikuwa nayo nchini Ivory Coast katika fainali za AFCON zilizopita

"Wachezaji wote wapo kwenye afya njema, hatutaki kufikiri mechi iliyopita, kule tumeshamaliza hakuna haja tena ya kuizungumzia, najua ni mechi ngumu tunakwenda kucheza dhidi ya Guinea, timu ambayo ilifanya vizuri AFCON iliyopita," alisema.



Naye kiungo wa timu hiyo, Novatus Dismas, alisema wamejifunza kutokana na mchezo uliopita kwani ulikuwa mgumu tofauti na walivyotegemea awali kama wachezaji, hivyo watakaza msuli ili kuhakikisha wanashinda mchezo ujao.

"Tumejifunza kutokana na mchezo uliopita, ulikuwa mgumu tofauti na tulivyotegemea, tumevifanyia kazi vitu ambavyo vilisababisha tukose ushindi mechi iliyopita, natumaini katika mechi inayokuja tutapata ushindi kwa sababu rekodi zinaonyesha tumekuwa tukipata matokeo mazuri tukicheza nje kuliko nyumbani,"alisema.

Mashabiki wengi wa soka walikosoa upangaji wa kikosi katika mchezo uliopita, wakidai kilikuwa na mabeki wengi zaidi kama vile timu ilikuwa inacheza ugenini na ilihitaji sare.

Kikosi cha Stars kiliondoka nchini usiku wa kuamkia jana kwenda Ivory Coast ambako mechi hiyo itachezwa, Uwanja wa Charles Konan Banny, Jumanne, saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.



Makamu wa pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hemedi Suleiman Abdulah (kulia) akikagua timu kwenye uwanja wa Jamhuri kabla ya kuanza kwa mchezo wa Mpira wa miguu wanaume Kati ya Mabingwa watetezi timu ya Uhamiaji dhidi ya Kikosi Maalum cha SMZ kwenye ufunguzi wa Michuano ya Majeshi yaliyoanza jana mkoani Morogoro. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Kocha Inter Z'bar atolea sababu kipigo

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya Inter Zanzibar FC, Abrahaman Mohamed amesema kupoteza mchezo wao wa kwanza wa Ligi kuu ya Zanzibar juzi kumetokana na ugeni wao kwenye Ligi hiyo.

Inter Zanzibar FC ilijikuta ikipokea kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa bingwa mtetezi, JKU SC, katika mchezo uliochezwa juzi katika uwanja wa New Amaan Complex Visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili, Mohamed alisema walicheza na timu yenye uzoefu mkubwa katika soka la Zanzibar lakini pia iliyopata kucheza mashindano mawili ya kimataifa hivi karibuni ' klabu Bingwa na Kagame cup'.

Alisema kupitia mashindano hayo walifanikiwa kupata maandalizi mazuri ya kujiandaa na msimu hivyo matokeo aliyoyapata hayawezi kumshangaza.

Alisema wachezaji wake walicheza vizuri katika kipindi cha kwanza lakini kipindi cha pili walishindwa kwenda sawa na wapinzani wao na kujikuta wakipata kipigo hicho.

"Wapinzani wetu walicheza kwa mipango kwa kutumia uzoefu wao ndani ya ligi jambo ambalo wachezaji wangu walishindwa kwenda nao sawa, tumefungwa kwa sababu ya ugeni wetu kwenye Ligi," alisema Mohamed.

Aidha alisema mbali na ugeni wa Ligi lakini pia wachezaji wake wengi walikuwa na hofu ya mchezo jambo lilowafanya kushindwa kucheza vizuri.

"Mchezo huu hatukufanya vizuri lakini kupitia mchezo huu nimeona mapungufu yapo wapi hivyo katika mchezo wetu wa pili dhidi ya Malindi SC tutakuwa bora zaidi," alisema.

Hata hivyo alisema kuwa kazi iliyombele yake katika kukiboresha kikosi chake ni kuhakikisha anawatoa uoga na hofu ya mchezo bila kujali historia ya timu wanayocheza nayo.

## Gamondi aiweka CBE kiganjani...

INATOKA UK. 24

kuwamalizia huku kwenye mchezo wetu wa nyumbani na kufuzu makundi," alisema Gamondi.

Mechi ya marudiano inatarajiwa kuchezwa Dar es Salaam kati ya Septemba 20 mpaka 22, ambapo mshindi kati ya timu hizo mbili atatinga hatua ya makundi.

## Fadlu aingia chimbo kuwasoma Walibya

INATOKA UK. 24

wachezaji wake ambao wamesema kwa sasa wana utimamu wa mwili tofauti na mechi za mwanzo za Ngao ya Jamii

"Kwa sasa nafurahi kwa utimamu wa mwili ambao wachezaji wangu wanao, na hii ni tofauti na ilivyokuwa kwenye michezo wa Ngao ya Jamii, ambapo wengi wao hawakuwa nao, pia hawakuwa na pumzi za kucheza kwa dakika zote 90,"alisema Fadlu.

Kwa mara ya kwanza, kocha huyo amefunguka juu ya tuzo ya kocha bora ya mwezi Agosti aliyoipata, alisema anashukuru sana, lakini kwake haitakuwa bora kama asipolishukuru benchi lake la ufundi na wachezaji wake kwa ujumla


"Tuzo ya kocha bora siyo ya kwangu tu, bali ya benchi lote la ufundi ambao wananisaidia nyuma kuandaa yote haya pamoja na wafanyakazi wengine, na wachezaji wangu ambao wamefanya kazi kubwa, fikiria tumefunga mabao saba, lakini hatukuwaacha wapinzani wetu wapige shuti hata moja lililolenga lango, hii inaonesha kuwa upande wa beki pamoja na kipa umefanyiwa kazi vizuri, lakini kule mbele tunatakiwa kuongeza juhudi, tumefunga mabao yetu matano baada ya mapumziko, lakini inatubidi tupambane zaidi," alisema kocha huyo.

Michezo
Jumapili Septemba 8, 2024
Nipashe



Depay atua Corinthians ya Brazil UK. 21

# GAMONDI AIWEKA CBE KIGANJANI MWAKE




## Amaliza kazi ya kuichambua na kuisoma mifumo yao, sasa anasubiri siku ya mchezo ili...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amemaliza kuwapeleleza wapinzani wake CBE, na sasa anasubiri siku ifike ili aoneshe kile alichokisoma kwao.

**Yanga itacheza mechi ya raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya timu inayomilikiwa na Benki ya Ethiopia, CBE, katika mchezo wa mkondo wa kwanza utakaochezwa, Uwanja wa Abebe Bikila, jijini Addis Ababa, Jumamosi ijayo.**

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kocha huyo ambaye alikuwepo Jumatano iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa katika mchezo kati ya Taifa Stars dhidi ya Ethiopia, pamoja na mambo mengine alikwenda kuwaangalia baadhi ya wachezaji wa CBE ambao wanaichezea timu yao ya taifa.

"Alifanya vitu viwili kwa wakati mmoja, alikwenda kuiangalia Stars, lakini alikuwa na majina na namba za mgongoni za wachezaji wa CBE wanaoichezea timu ya taifa, lengo ni kuangalia viwango vyao na jinsi wanavyocheza ili iwe rahisi kuwaelekeza wachezaji wa Yanga jinsi ya kukabiliana nao," alisema mtoa taarifa.

Baada ya mchezo huo, Gamondi hakutaka kuongea chochote na waandishi wa habari.

mbali na hilo, habari zinasema alimtuma mmoja kati ya wachambuzi wa video kwenda kuangalia michezo miwili kati ya CBE na SC Villa ambayo ilichezwa nchini Uganda, Uwanja wa Mandela, Agosti 17 na Abebe Bikila uliopigwa Agosti 24.

Katika mchezo wa kwanza ikiwa ugenini, CBE ilishinda mabao 2-1, na mechi ya marudiano nyumbani ilitoka sare ya bao 1-1.

"Alitumwa mtaalam kuangalia mechi hizo kwa sababu yoyote ambaye angeshinda angekutana na Yanga, na baada ya CBE kupita kazi ilianza ya kuichambua jinsi inavyocheza, kizuri zaidi na baadhi ya wachezaji wao wamekuja hapa na kikosi cha Ethiopia, mwenyewe alikwenda kuwaangalia.

Kwa maana hiyo tayari ameshaifahamu timu hiyo jinsi inavyocheza na nini anatakiwa afanye yeye na wachezaji wake," kilisema chanzo hicho.

Hivi majuzi, Gamondi alisema watakwenda kucheza ugenini kwa tahadhari na kuwadhibiti wapinzani wao ili wasipate ushindi kabla ya kuwamalizia nchini Tanzania.

"Tukimaliza kuwapeleleza, tutakwenda kucheza mechi ya kwanza ugenini, tutajaribu kuwadhibiti kwanza kwao, tukifanikiwa kuwasukuma na kuwadhibiti ili wasitufunge, tutakuja

INAENDELEA UK 23

# Fadlu aingia chimbo kuwasoma Walibya

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, ameanza kazi ya kuifuatilia timu ya Al Ahly Tripoli ya Libya kujua habari zao na jinsi wanavyocheza ili kuwa na kazi rahisi ya kuidhibiti katika mchezo wa mkondo wa kwanza wa raundi ya kwanza Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa Juni 11, jijini Tripoli, Jumapili ijayo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Fadlu, raia wa Afrika Kusini, alisema ameshaanza kuwasoma wapinzani wake ingawa bado anaendelea kuchimbua taarifa zao, uchezaji wao na mifumo wanayotumia ili iwe rahisi kukabiliana nao.

"Maandalizi hayajaisha, yanaendelea, tuna mambo mengi ya kufanya, kujiandaa sisi wenyewe mazoezini, lakini pia kuwasoma wapinzani wetu pia, ni siku chache tu tutaondoka kwenda kuwakabili.

Hatujapata kila kitu kutoka kwao, ila tuna taarifa chache ambazo zinaweza kutusaidia pa kuanzia, lakini tunaendelea kuwasoma na kupata taarifa zao nyingi," alisema kocha hiyo.

Akiizungumzia mechi hiyo, Fadlu alisema itakuwa ngumu kutokana na Walibya hao wana timu nzuri, itakayocheza mbele ya mashabiki wao ambao kwa sasa wameruhusiwa kuingia viwanjani.

"Tuna mechi ngumu dhidi ya Al Ahly Tripoli nyumbani kwao, tunacheza mbele ya mashabiki wao ambao najua watawashangilia sana, lakini sisi hivi karibuni tulicheza mechi ya majaribio dhidi ya Al Hilal ya Sudan, imetusaidia sana, ulikuwa mchezo mzuri na kipimo tosha kwetu, imetuonyesha levo ya ushindani ambayo tunayo mpaka sasa," alisema.

Licha ya kwamba katika mchezo huo walitoka sare ya bao 1-1, lakini alifurahishwa na maendeleo ya

INAENDELEA UK 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >